SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 4

## MBOWE aja kivingine kujenga CHADEMA mpya




Jumatatu Aprili 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580912
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kinana akemea viongozi wanaotaka kutukuzwa



**ASEMA** kazi nzuri ndiyo inayotukuzwa, kuanza ziara mikoani...*Endelea Ukurasa 2*



Kutokana na mvua inayoendelea kunyesha katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea imebomoa daraja linalounganisha kata za Matarawe na Mjimwema Mkoani Ruvuma na kusababisha adha kubwa kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma za Afya katika Kituo cha Afya cha Mjimwema. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**



Waamini wa Kanisa la Anglikana Kristo Mfalme Kinondoni, Dar es Salaam wakiandamana kuadhimisha Sikukuu ya Matawi, jana ndiyo mwanzo wa Juma Kuu linaloadhimishwa jinsi Yesu Kristo alivyoingia mara ya mwisho Yerusalemu ili kufa na kufufuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ripoti ya CAG kuumbua ‘vigogo’

UKURASA 3

## Madarasa 12 ya UVIKO-19 yapasuliwa vioo

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA HAWATANII KWA ORLANDO UK.23
MAONI, KATUNI UK.6




Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa akiwa na Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa Benki ya CRDB, Chiku Issa (wa pili kushoto) wakikabidhi vyakula kwa kituo cha wenye uhitaji cha Imani Chumbageni ikiwa ni sehemu ya mchango wa Benki ya CRDB kwa kituo hicho katika mfungo wa mwezi Ramadhani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinana akemea viongozi wanaotaka kutukuzwa

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Bara, Abdulrahman Kinana, amekemea tabia ya baadhi ya viongozi kutaka utukufu, huku akiwataka kufanyakazi itakayoonekana kwa wananchi ili watukuzwe kwa kazi yao nzuri.

Aidha, alisema kwa muda atakaokuwa kwenye nafasi hiyo atatanguliza utumishi na siyo utukufu, huku akiahidi kuwa mwadilifu na mwenye bidii na kwamba ataanza ziara kwenye mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro na Arusha itakayofuatiwa na mikoa saba baadaye.

"Nitatanguliza utumishi na siyo utukufu, maana yake hivi karibuni hivi vyeo tunavyovipata nchini siku hizi nikitiza tizama kuna mila na desturi inaanza ya vyeo kuendana na utukufu na mbwembwe nyingi, nawaomba wenzangu mjue kuchaguliwa, kupewa nafasi ya uongozi ni utumishi wa umma,"alisema na kuongeza:

"Watakao kutukuza ni wale unaowatumikia, ukifanya kazi vizuri watakutukuza, ukijitukuza mwenyewe watakushusha."

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam wakati akihutubia katika hafla ya kumkaribisha mkoani humo, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumpendekeza na wana CCM kumchagua kwa kura nyingi kutumikia nafasi hiyo, huku akiwaahidi atatimiza majukumu yake kwa weledi bila kuwaangusha.

"Nishukuru wana CCM kwa kunichagua, niwaahidi chama chenu kina waheshimu, kina wathamini na kitakuwa karibu na nyinyi ili kiwe imara na kuchaguliwa zaidi kila uchaguzi unapofika," alisema Kinana.

Aidha, aliwasihi viongozi wa CCM ngazi za taifa, mikoa na wilaya, kujifunza kutoka kwa mabalozi wa mashina na kata namna ya kukitumikia chama hicho kwa kujitolea, huku akimpongeza katibu mkuu, wakurugenzi, wakuu wa wilaya, madiwani watumishi wa halmashauri na wenyeviti wa kazi nzuri wanazofanya. Kinana alisisitiza kuwa kila mwanachama wa chama hicho ana nafasi na haki ya kuchaguliwa na kuchagua ndani ya CCM, huku akiwataka vijana na wakina Mama kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi zinapojitokeza.

Vile vile, alisema mafanikio makubwa yanayoonekana yanatokana na uongozi mzuri wa Rais Samia akieleza kuwa ana maono mazuri ya kiuchumi na kisiasa kwa kujenga demokrasia ya maridhiano, kuheshimiana na yenye kujenga amani na utulivu ndani ya nchi akisisitiza wana CCM na watanzania kwa ujumla kumuunga mkono.

"Nina hakika tukimuunga mkono Rais tutapiga hatua kubwa sana, na mimi nitakuwa naye, nitamuunga mkono na nitashikamana naye kuhakikisha tunatekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM, ili wananchi waweze kupata mafanikio makubwa, lazima tuisaidie serikali iweze kutimiza wajibu wake, najua wananchi wanataka nini wanasema nini wananung'unika juu ya kitu gani lazima tuyajadili ili kupata ufumbuzi," alisema Kinana.

**OMBI KUIGAWA ILALA**

Awali, Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, alimuomba Kinana kuwasemea katika ngazi ya taifa kuhusu kuigawa wilaya ya Ilala kwa kuwa ni kubwa.

"Mkurugenzi wa Ilala anavyofanya kazi kutoka hapa mpaka Kata ya Zingiziwa ni kazi kubwa, kwa hiyo ninadhani ili kutusaidia ifanyike hivyo viongozi wawe karibu na watu ili na wao waende kwa (speed) kasi kama Ubungo, Temeke, Kinondoni na Kigamboni kwasababu ni jiji, lakini kuna eneo ni manispaa sasa kazi ya Kumbilamoto ni kubwa sana.

"Tusaidiane ili Ilala iende vizuri, nimeona nilichomekee hili na wewe ni makamu mpya basi inaweza ikawa ni moja ya zoezi lako la kwanza kutusaidia sisi wana Dar es Salaam," alisema Kate.

**CHONGOLO ATAJA CHANGAMOTO**

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Daniel Chongolo, alisema walikuwa na changamoto ya kuwa na wajumbe wachache katika vikao vyao vya maamuzi hasa mikutano mikuu, halmashauri kuu za ngazi mbalimbali, ambao ndiyo huchagua viongozi wanaowakilisha serikali, lakini kwa sasa wamepanua wigo kwa kuchukua mwenyekiti na katibu wa kila jumuia kuanzia kwenye tawi ili kushiriki katika mikutano hiyo.

"Lengo ni kuongeza wigo wa maamuzi ili makundi haya yashiriki katika kuamua viongozi katika maeneo yao na mambo ya msingi ya sehemu husika, pia mwaka huu tunafanya uchaguzi wa ndani lakini niseme uchaguzi na nafasi ndani ya chama chetu hazina umiliki wala hati miliki ya mtu mmoja, hakuna mtu mwenye haki zaidi ya mwingine sote ni sawa, ni haki ya mwanachama kikatiba kujitokeza kujipima, usiogope,"alisema na kuongeza:

"Kumekuwa na katabia sasa hivi mtu anaanza kufikiria mambo ya 2025 anaangalia anaanza kuota ubunge, udiwani. Wabunge, madiwani tunao chama hakina uhaba mpaka 2025, acheni kupanga safu na kupanga watu, mwanasiasa mzuri hahangaiki kutengeneza watu kwa mambo ya mbeleni, wajanja huwa wanahangaika siku ikifika, mwanasiasa mzuri ni yule anayehangaika na jambo wakati muafaka."

# Shule sekondari iliyojengwa kwa fedha UVIKO -19 yavunjwa vioo madarasa 12

**Na Idda Mushi,** GAIRO

MKUU wa Shule ya Sekondari Kibedya, wilayani Gairo mkoani Morogoro, Kelvin Kayombo, amesimamishwa kazi kupisha uchunguzi baada ya madarasa 12 yaliyojengwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19, maarufu kama madarasa ya Mama Samia, kuhujumiwa kwa kuvunjwa vioo.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabir Makame, alisema hayo wakati akizungumza na wananchi kwenye Kijiji cha Itaragwe.

Alisema amelazimika kumuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo kumsimamisha kazi mkuu huyo kupisha uchunguzi na kuchukua hatua zingine ikiwamo kukamatwa kwa watu watatu wanaotuhumiwa kuhusika na tukio hilo akiwamo mlinzi wa shule hiyo.

"Tulimhoji mlinzi wa shule na mbele ya kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya, alikiri siku ya tukio hakuwapo eneo lake la kazi, lakini mbaya zaidi shule imefungwa miundombinu ya umeme, siku ya tukio hakukuwa na umeme, kumbe Luku imeisha muda mrefu na uongozi wa shule haukuhangaika kununua," alisema Makame.

Licha ya kukamatwa kwa watu hao na kusimamishwa kazi kwa mkuu wa shule, Mkuu wa wilaya pia ameagiza watu wote waliohusika na uharibifu huo kulipa gharama za kuweka upya vioo vilivyovunjika, wakati mashauri yao yakiendelea kwenye vyombo vya dola.

Aliwataka wananchi kila mmoja kutambua wajibu wake wa kuwa mlinzi wa mali za umma na tukio hilo limeleta fedheha kubwa ikizingatiwa Wilaya ya Gairo pekee ilipokea Sh. bilioni 1.1 kutoka kwenye mpango huo.

"Madarasa yaliyojengwa yaliwezesha wanafunzi wote waliofaulu darasa la saba mwaka jana Gairo nzima kuendelea na masomo kwa wakati mmoja, Kibedya peke yake walipokea Sh. milioni 120 kwa ajili ya madarasa sita," alisema.

Mwandishi wa habari hizi alifika katika shule hiyo na kushuhudia uharibifu wa vioo katika madarasa 12 yaliyogharimu zaidi ya Sh. milioni 120 kwa kuvunjwa vunjwa vioo, taarifa ambazo ziliripotiwa pia kwenye kikao cha dharura cha Baraza la Madiwani.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Gairo, Shaban Sajilo, amelaani kitendo kilichofanywa.

"Ufanyike msako wa uhakika, na mtu huyu akishakamatwa tuone asilimia 100 ya sheria inafuata mkondo wake, kusiwapo na huruma hata kidogo, huyu ni sawa na mhaini au mhujumu uchumi," aliwaambia madiwani.

Diwani wa kata ya Kibedya, Butindi Masatu, alisema wahusika wote waliofanya tukio hilo wanatakiwa kusakwa na kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria, na kwamba walipewa madarasa sita na madirisha yote ya nyuma yameharibiwa.

"Tuhamasishane ili kila mmoja alipo aweze kumjua jirani yake ni wa aina gani, anatoka wapi na anafanya kitu gani," alisema Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Augustino Nicholaus.

Taarifa zisizo rasmi zinadai kuwa kuvunjwa vioo hivyo kumetokana na wivu wa kimapenzi baada ya mtuhumiwa kumtuhumu mlinzi wa shule kuwa na mahusiano na mkewe, hoja ambayo licha ya kutajwa na viongozi na wanakijiji, imeshindwa kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilim.

Baadhi ya wananchi wa Gairo, Hellena Mwangila na Charles Madenge, wamelaani tukio na kusema hata kama kulikuwa na ugomvi binafsi, haukupaswa kuhusishwa na mali za umma, kwa kuwa madarasa hayo yanalenga kusaidia kuinua na kuboresha kiwango cha elimu kwa wananchi wote bila ubaguzi.

HABARI KITAIFA

# Ripoti ya CAG kuumbua 'vigogo' wa umma wiki hii

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

JUMA hili litakuwa gumu kwa baadhi ya viongozi wa mashirika na taasisi za serikali ambao 'watаumbuka' kutokana na ama kufuja mali ya umma au kushindwa kutimiza majukumu yao kikamilifu.

Kwanini? Rais Samia Suluhu Hassan kupitia wasaidizi wake, ana siku nne pekee kuanzia leo kuhakikisha anaiwasilisha bungeni ripoti ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2020/21 aliyokabidhiwa Machi 30, mwaka huu.

Hilo linatokana na masharti yaliyoko kwenye Ibara 143 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Inatamkwa kwenye Ibara ya 143(4) ya Katiba hiyo kuwa: "Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kilipoanza kikao hicho."

Mkutano wa Bunge la Bajeti ulioanza Jumanne Aprili 5, leo unaingia katika kikao (siku) chake cha nne. Alhamisi hapakuwa na kikao kutokana na sikukuu ya Kumbukumbu ya Karume, ripoti ya CAG itawasilishwa bungeni ndani ya siku nne kuanzia leo ili kukidhi matakwa ya kikatiba (siku za mwishoni mwa wiki na sikukuu hazihesabiki).

Baada ya kuwasilishwa bungeni na mawaziri husika, Ripoti ya CAG itakuwa wazi kwa umma na kwa taratibu za Bunge, itakabidhiwa kwa kamati zenye mamlaka ya kuifanyia uchambuzi ambazo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Miongoni mwa hoja zinazotarajiwa kuwa gumzo katika ripoti ya CAG ni madai ya uwapo wa ufisadi katika miradi inayosimamiwa na taasisi na mashirika ya umma na 'mchwa' wa fedha za maendeleo katika halmashauri mbalimbali hasa mikoa yenye miradi mikubwa.

Hoja nyingine ni hali ya Deni la Taifa, kuendelea kuwapo kwa watumishi na wastaafu hewa, malipo kwa vifaa na miradi 'hewa', hali ya miundombinu ya magereza nchini na hali ya utumishi kwa maana ya uhaba wa watumishi kwa tafsiri yake pana.

**ALICHODOKEZA CAG**

Alipokabidhi kwa Rais Samia ripoti hiyo, CAG Charles Kichere, alisema ameangazia utendaji wa vyama vya siasa, hali ya mifuko ya hifadhi ya jamii na utendaji wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) waliotozwa riba ya mabilioni ya shilingi kwa kuchelewesha malipo ya madeni ya makandarasi na washauri wa ujenzi Sh. bilioni 673.52.

CAG alisema ripoti imegusa hali ya viwanja vya balozi mbalimbali za Tanzania ambavyo havijaendelezwa huku serikali ikitumia Sh. bilioni 3.6 kwa mwaka kukodi nyumba kwa ajili ya balozi zake 10.

Ripoti hiyo pia imemulika utendaji wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), ambayo imetajwa kushindwa kuwahudumia ipasavyo wateja wa ndani ilhali iko zabuni ya kusambaza dawa kwa wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Vilevile, alisema amemulika madeni chechefu kwenye benki, pia akaunti za taasisi za umma 68 hazikuwasilisha Benki Kuu (BoT) Sh. bilioni 148.81, Dola za Marekani milioni 6.33 na Euro milioni sita.

CAG pia amekagua upakuaji wa meli za mizigo, akibaini zinakaa muda mrefu bandarini; kuchelewa kuunganisha umeme kwa wateja wa Shirika la Umeme (TANESCO); mkataba wa Symbion ambao alibaini TANESCO ilikosa umakini katika kuusitisha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani milioni 153.43.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu huyo pia ameanzisha ukaguzi mpya wa fedha zinazolipwa na watuhumiwa kupitia sheria mpya ya kukubaliana na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kukiri kosa na kulipa pamoja na mali zilizotaifishwa baada ya kesi mahakamani.

Katika ripoti hiyo, CAG pia amekagua miradi mikubwa ya kimkakati, akibaini kuchelewa kwa mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, vichwa vya treni na mabehewa kuchelewa kuwasili kwa ajili ya majaribio ya mradi wa reli ya kisasa (SGR).

CAG pia amebaini mashirika 38 hayana bodi. Kati yake, 26 yanafanya kazi bila bodi kwa miaka 12, huku mikopo itokanayo na asilimia 10 ya makusanyo ya halmashauri haijarejeshwa kwenye mamlaka za serikali za mitaa 155.

CAG atakapokutana na waandishi wa habari wiki hii kutoa mukhtasari wa ripoti yake hiyo, anatarajiwa kubainisha maendeleo ya ukaguzi maalum anaoufanya kuhusu matumizi ya fedha za mkopo wa Sh. trilioni 1.3 za kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19.


## TAARIFA KWA UMMA



**MUSA CHARLES NG'OGELA**

Mtajwa hapo juu anatafutwa na mwajiri wake **FURAHA NYANZA CO LTD** na police kwa tuhuma za kumuibia mwajiri wake.Yeyote atakayemuona au mwenye taarifa ya mahali alipo azitoe kituo chochote cha polisi kwa kutumia RB Namba NY/RB/1501/2022 au kwa kupiga simu kwa mwajiri wake **0763835368.**

Yeyote atakayefanya nae Biashara au Makubaliano kwa niaba ya Kampuni hii, Kampuni haitahusika kwa namna yeyote ile na Biashara hiyo au makubaliano hayo.

*Zawadi nono itatolewa kwa atakayefanikisha kupatikana kwake.*

116797202


# Hoja nyeti kujibiwa bungeni keshokutwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

HOJA nyeti zilizoibuliwa na wabunge wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka ujao wa fedha, zinatarajiwa kupatiwa majibu na serikali wakati wa kuhitimisha mjadala huo keshokutwa.

Mjadala huo ulianza Jumatano iliyopita baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwasilisha makadirio hayo bungeni jijini hapa, wabunge waliwasilisha hoja mbalimbali ikiwa ni pamoja na tatizo la uhaba wa ajira nchini na watumishi wa umma kutopandishwa mishahara kwa miaka sita mfululizo huku wenzao wa sekta binafsi wakishuhudia kutorekebishwa kwa kima cha chini cha mshahara kwa takriban miaka 10.

Hoja zingine katika mjadala huo ni: kupanda kwa kasi bei ya bidhaa nchini; ombi la kuruhusu uagizaji huria wa mafuta uende sambamba na uagizaji wa pamoja wa nishati hiyo katika kipindi hiki ambacho vita vya Russia na Ukraine vimesababisha kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo duniani; na kumulika kiini cha ucheleweshaji wa upakuaji wa mizigo bandarini.

Kwa mujibu wa ratiba ya Mkutano wa Bunge la Bajeti iliyotolewa na Idara ya Habari na Elimu ya Bunge wiki iliyopita, mjadala huo utaendelea leo hadi utakapohitimishwa kwa serikali kujibu hoja zilizoibuliwa.

**KIKOKOTOO CHA MAFAO**

Wakati mjadala huo ukiendelea wiki hii, kunatarajiwa kuibuka hoja ya serikali kueleza hatua iliyofikiwa katika mchakato wa kuwa na kikokotoo kipya cha mafao ya watumishi wa umma, suala lililoibua mjadala mkali wa kitaifa miaka minne iliyopita.

Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, aliingilia kati suala hilo, akiagiza kikokotoo kipya cha mafao kianze kutumika mwaka 2023.

Wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka huu wa fedha (2021/22), Waziri Mkuu Majaliwa alisema kumeundwa kamati maalum ya kuratibu mchakato wa kupata kikokotoo kitakachokubalika kwa watumishi, pia kushirikisha wadau katika kukipata.

Ratiba ya mkutano huo wa Bunge pia inaonyesha Alhamisi kutawasilishwa bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais na taasisi zake na kwamba mjadala wake utafanyika kuanzia siku hiyo hadi Ijumaa Aprili 22, mwaka huu.

Hoja zinazotarajiwa kuibuka ni pamoja na uhaba wa watumishi, hasa kwenye Sekta za Afya na Elimu ilhali mitaani kuna wahitimu wengi wa vyuo vikuu na vya kati wenye mafunzo ya kada hizo.


## CONTRACTORS REGISTRATION BOARD

## REGISTRATION STATUS UPDATE

The Board would like to inform all contractors registered in **CLASS FIVE** as of 30.06.2017 that Pursuant to section 4(q) of the Contractor Registration Act No. 17 of 1997, it is now updating contractors' information in the database to match with the current status of the contractor in terms of shareholding status, official addresses, staffing level and equipment holding capacity.

In order for the said information to be effectively and timely updated, the said contractors are hereby instructed to submit the duly filled **REVIEW INFORMATION FORM (already posted in your postal addresses and can also be downloaded on the website www.crb.go.tz**).

In addition, the following information should be submitted along with the said form:

1. Current Business Registration and Licensing Authority (BRELA) Search Report.
2. Covering letter indicating inter alia, which names among the shareholders shown in the Brela search, stands as Managing and Technical Director in the construction company.
3. Resolution of the Board of Directors and Affidavit as a commitment that the submitted information is correct and can be used to update your company status in the data base.

The said information should reach the Board latest by 30th April 2022.

**REGISTRAR**

216795702



Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, akipokea fedha kutoka kwa mmoja wa wananchi eneo la Kata ya Wazo, Jimbo la Kawe, Dar es Salaam, katika ziara ya mguu kwa mguu 'join the chain', kwa lengo la kupata fedha za kujenga chama hicho. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mbowe sasa aja kivingine kuijenga CHADEMA mpya

**Na Jenifer Gilla**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema moto wa siasa umewashwa ndani ya chama hicho, huku akiahidi kufanya kazi usiku na mchana kuwafikia watanzania.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yake jimbo la Kawe, ikiwa ni kampeni ya mguu kwa mguu kuzungumza ana kwa ana na wananchi pamoja na kukusanya fedha za kujenga chama.

Mbowe alisema ziara hiyo ni mwendelezo wa oparesheni ya 'join the chain' yenye lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa chama hicho pamoja na kutoa elimu ya uraia kwa wananchi.

Akizungumza na wananchi wa Tegeta na kata ya Kunduchi, Mbowe alisema matembezi hayo yatakuwa ni kwa miguu ndani ya mitaa ya jiji hilo, na kwamba pamoja na mambo mengine ni kuwashukuru Watanzania kwa kupigania uhuru wake alipokuwa gerezani.

"Na ninatembea kama mnavyoniona kuwasalimia wananchi, nikitambua namna mamilioni ya Watanzania walivyolilia uhuru wangu na vijana wangu nilipokuwa gerezani. Kwa hiyo napita kuwasalimia kuwashukuru namna ambavyo mlitetea haki yetu na uhuru wetu, asanteni sana na Mungu awabariki," alisema Mbowe.

Mbowe aliongeza kuwa kazi ya siasa haijafika mwisho bali imechochewa moto kwa kuwa chama hicho kitatembea usiku na mchana kuhakikisha kuwa wanaliamsha taifa ili litambue namna ya kutetea watu wake.

"Tutatembea usiku na mchana, kwa jasho na damu, kuhakikisha tunaliamsha taifa hili, lijitambue ,lijue namna ya kutetea haki na uhuru wa nchi yake, namna ya kuibana serikali yetu itambue kwamba maisha ya wananchi yamekuwa magumu, waache kuongeza tozo, ili maisha ya wananchi yawe nafuu," alifafanua.

Kwa mujibu wa Mbowe, wajibu wa kulitetea taifa ni wa kisiasa na kuwataka wananchi wa Tegeta kumuunga mkono katika wajibu huo ili kupaza sauti kwa pamoja.

"Lazima tupaze sauti yetu, hatuwezi kuendelea kuwa taifa la kuoneana, kudhulumiana, la kunyanyasana na taifa la ubaguzi wa kiitikadi. Asanteni Kawe kwa mapokezi mazuri, Tegeta nitaendelea kuwa na ninyi,hakuna kulala mpaka kieeleweka," alisema.

Aidha, baada ya kuzungumza Mbowe alianza kukusanya michango ya hiyari kutoka kwa wananchi hao kwa ajili ya kusaidia kujenga chama huku akisisitiza kuwa kitajengwa na wananchi wenye uwezo mdogo ambao hutoa fedha zao kama sadaka ya ukombozi na siyo matajiri pekee.

# Rais Samia awapandisha vyeo Makamishna TAWA

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewapandisha vyeo makamishna wasaidizi waandamizi watano na makamishna wasaidizi 12 wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA),

Hafla hiyo iliyofanyika makao makuu ya ofisi hizo mkoani Morogoro, imefanywa na Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya TAWA, Meja Jenerali mstaafu Hamisi Semfuko, kwa niaba ya Rais Samia.

Meja Jenerali mstaafu Semfuko, aliwaasa maofisa hao kujitambua kuwa sasa wako kwenye nafasi zaidi ya kufikiri na kupanga na wawe tayari wakati wote kupangiwa majukumu zaidi kiutawala na kuwahimiza kuwa wazalendo na kuifahamu nchi na siasa zake na viongozi waliopo.

Alisema jeshi hilo lipo kwa mujibu wa sheria na ni moja ya vyombo vilivyo chini ya usimamizi wa Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi la Ulinzi na usalama wa nchi, na hiyo ni fursa adhimu.

"Makamanda na wapiganaji, nataka pia mjue kuwa bodi katika kutekeleza hili imeangalia sana utulivu na uwezo wenu, kumekuwa na uwazi mkubwa kufikia hatua hii mliyofikia, ni imani yetu kwamba kuanzia sasa mtabadilika kwa vitendo vyenu vya binafsi, lazima muwe mfano katika mazingira yote, ya ndani na nje," alisisitiza.

Semfuko akawahimiza kuwa na weledi mkubwa katika majukumu yao na kukumbuka katika jeshi, viongozi wa ngazi mbalimbali wanapaswa kujua uwezo wa walio chini yao na walio juu yao, matatizo na shida zao na kuona namna ya kuwadhibiti.

Alimshukuru waziri aliyemaliza muda wake, Dk. Damas Ndumbaro kwa uongozi mahiri katika wizara ya Maliasili na Utalii uliooonesha mafanikio makubwa na kumpongeza waziri mpya Dk. Pindi Chana na kuahidi kwamba bodi na wakurugenzi katika mamlaka hiyo watampa ushirikiano.

Kamishna Mkuu wa Uhifadhi TAWA, Mabula Nyanda, alisema jitihada wanazoendelea kufanya ni kwenye mafunzo na uboreshaji wa vitendea kazi vya kijeshi ikiwamo magari, bodi, miradi 32 ya UVIKO inayoendelea na mazingira bora zaidi ya ufanyaji kazi.

Baadhi ya wajumbe wa Bodi ya TAWA, Meja Jenerali mstaafu George Msongole ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uhifadhi, Dk. Fabian Madelle, Mwenyekiti wa Kamati ya Rasilimali watu na uendeshaji pamoja na Katibu Tawala wa wilaya ya Morogoro, Ruth Magufuli, walihimiza maofisa hao kutambua hakuna ofisa kwenye Jeshi kiutendaji na kwamba hawana budi kufanya kazi kwa bidii zaidi na maarifa kufikia mafanikio.

Walihimiza kuimarisha nidhamu na uwajibikaji wa askari pamoja na ukakamavu ili kufikia malengo ya mamlaka hiyo na kuwa na jeshi imara na lenye nidhamu na uadilifu.

# Mbaroni tuhuma kumnajisi mtoto wake wa kambo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Ndala Manispaa ya Shinyanga (26) ( jina limehifadhiwa), anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wake wa kambo mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi 11.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, alisema tukio hilo limetokea juzi, saa 8:30 mchana.

Alisema mtuhumiwa alimnajisi mtoto huyo wakati mama yake akiwa ameenda dukani, na kisha kumsababishia maumivu sehemu zake za siri na kutokwa damu.

"Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga tunamshikilia mwanaume mmoja mkazi wa Ndala Manispaa ya Shinyanga kwa kosa la kumbaka (kumnajisi) mtoto wake wa kambo," alisema Kyando.

Aidha, alisema upelelezi bado unaendelea, na kwamba mtuhumiwa akikutwa na hatia atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Katika hatua nyingine Kamanda alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa huo wa Shinyanga kuacha kufanya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

# 100 wanaswa tuhuma za kuishi nchini kinyemela

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

IDARA ya Uhamiaji wilayani Kahama mkoani Shinyanga imewakamata raia wa kigeni 100 kwa tuhuma za kuingia nchini kinyemela.

Watuhumiwa hao kutoka nchi tano, walikamatwa katika msako uliofanyika Machi 24, mwaka huu .

Waliokamatwa ni kutoka nchi za Burundi, Rwanda, Kenya, Nigeria na Ghana, huku baadhi yao wakirudishwa makwao na wengine wakifikishwa katika vyombo vya sheria.

Ofisa Uhamaji Wilaya ya Kahama, Salumu Rashidi, alisema wahamaji kutoka Kenya walikuwa wawili, Nigeria (1), Ghana (1) na wengine wakitoka Burundi.

Alisema kuwa wahamiaji hao walikamatwa katika oparesheni ambayo ilifanywa na Uhamiaji lengo likiwa ni kuwakamata ambao walikuwa wakiishi nchini bila ya kufuata utaratibu.

Aidha Rashidi alisema watatu kutoka Burundi walihalalishwa ukazi na kuongeza kuwa waliobakia walirudishwa nchini kwao kupitia mpaka wa Kabanga, huku akisisitiza kuwa wananchi waache kuwamiliki wahamiaji hao bila ya kufuata sheria.

Hata hivyo Rashid alisema maeneo ambayo wahamiaji hao haramu walikamatwa katika msako huo ni Kakola, Isagehe, Ushetu na eneo la Kagongwa lililopo katika Manispaa ya Kahama.

Alitoa wito kwa wananchi kuacha kuwamiliki wahamiaji haramu kinyume cha sheria hasa watoto na kuongeza kuwa atakaebainika anafanya hivyo faini yake ni Sh. milioni 5- 20 pamoja na kuambatana na kifungo.



Wanafunzi wa Umoja wa Vyuo Vikuu AIESEC wakipata maelezo na huduma mbalimbali zinazotolewa na Benki ya CRDB walipotembelea banda la benki hiyo wakati wa kongamano la AIESEC, lenye lengo la kuwajengea vijana uwezo wa kukabiliana na ushindani na changamoto mbalimbali katika soko la ajira pindi wamalizapo masomo yao. CRDB Benki ni mshirika katika umoja huo wa elimu ya vyuo vikuu nchini.

# ZAECA yachunguza malalamiko dhidi ya mwekezaji sekta utalii

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) imeanza kuchunguza malalamiko ya mwekezaji wa kampuni ya Pilipili inayodaiwa kushindwa kulipa wafanyakazi zaidi ya 800 na wasambazaji wa vyakula 80 katika hoteli 17 anazoziendesha.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Makarani Ahmed Makarani, alisema amepokea malalamiko dhidi ya muwekezaji huyo kuwa hajawalipa wafanyakazi mishahara pamoja na wafanyabiashara waliokuwa wakitoa huduma za vyakula katika hoteli hizo.

"Ni kweli tunaendelea na uchunguzi, wafanyakazi 800 hawajalipwa mishahara yao pamoja na wasambazaji wa bidhaa wapatao 80 wakidai viwango tofauti vya fedha baada ya kutolipwa kwa muda mrefu,"alisema Makarani.

Alisema kazi inayofanyika ni kuhakikisha wafanyakazi hao wanalipwa stahiki zao pamoja na wasambazaji wa bidhaa, huku mamlaka ikiendelea kuchunguza makosa mengine ya jinai kama kutolipa kodi Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na michango ya wafanyakazi katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

Mmiliki wa Hoteli ya Uhuru Beach, Anne Petricia Down, alisema ameamua kuvunja mkataba wa uendeshaji wa hoteli hiyo na mwekezaji kutoka Poland, Wojciech Zabinski, kutokana na kushindwa kuheshimu masharti ya mkataba.

Alisema wafanyakazi katika hoteli hiyo hawajalipwa mishahara kwa miezi miwili pia michango yao haijawasilishwa ZSSF na kutolipa kodi ZRB.

"Nimekodisha hoteli yangu kwa miaka 10 mpaka sasa ni miaka miwili matatizo yamekuwa mengi, watu wanajitokeza kudai fedha baada ya kusambaza bidhaa za vyakula bila kulipwa," alisema Anne, Raia wa Uingereza.

Alieleza kuwa ameshaandika barua ya malalamiko, Kamisheni ya Utalii Zanzibar ili kuingilia kati kufanikisha kupata hoteli yake iliyopo katika eneo la Jambiani Mkoa wa Kusini Unguja.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Rashid Makame Shamsi, alisema wafanyakazi na wasambazaji wa vyakula walianza kujitokeza mmoja mmoja, lakini mpaka sasa wamebaini wafanyakazi zaidi ya 700 wanadai stahiki zao na wasambazaji wa vyakula ni zaidi ya 800.

"Natayarisha ripoti na imefikia hatua kubwa, kabla ya kukabidhi Kamisheni ya Utalii na mamlaka zingine za serikali... ninachowaomba wafanyakazi wanaodai stahiki zao pamoja na wasambazaji wa bidhaa kuwa na subira wakati serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hilo,"alisema.

Aidha alisema kuna baadhi ya wamiliki wa hotali kati ya hoteli zilizokodiwa na mwekezaji huyo wanalalamika kutolipwa fedha zao za ukodishaji na kuamua kuanza mchakato wa kudai kurejeshewa hoteli zao.

Wakizungumza na waandishi wa habari baadhi ya wafanyakazi wa hoteli ya Uhuru Beach walisema wapo wanaodai mishahara kati ya miezi mitatu na wengine miwili pamoja na fedha walizokuwa wakikatwa katika mishahara yao, lakini haziwasilishwi ZSSF.

"Nilikwenda kuangalia mafao yangu ZSSF nilijibiwa hakuna mchango uliongia tokea nianze kazi kabla ya kusimamishwa, huku nikidai mshahara wa miezi mitatu,"alisema mmoja wa wafanyakazi hao ambae hakutaka kutajwa jina.

"Mimi binafsi nadai milioni 53 kwa kusambaza bidhaa za vyakula, matunda na mboga"alisema Ramadhan Abdallah Ameri.

Msambazaji wa samaki, Ramadhan Hassan, alisema anadai Sh. milioni 38 kutoka kwa mwekezaji huyo, lakini amekuwa akimpiga chenga kumlipa na kutoa ahadi bila kutekeleza.

Hata hivyo, viongozi wa kampuni ya Pilipili akiwamo mwekezaji huyo, hawakutaka kuzungumza na waandishi wa habari walipofika katika hoteli hiyo huko Jambiani.

Orodha ya wasambazaji 24 wa bidhaa za aina mbalimbali inaonyesha kuwa wanadai Sh. milioni 822.4 kati ya wasambazaji 80 wanaomdai muwekezaji huyo. Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Mbamba, alisema kamisheni hiyo kazi yake ni kutoa leseni za hoteli, masuala ya kazi na biashara yanasimamiwa na mamlaka zingine.

# Prof Ngowi: Lazima ujue kutofautisha gharama na faida

**Na Jenifer Gilla**

MIAKA mitatu iliyopita, katika moja ya vipindi vyake, marehemu Profesa Honest Ngowi, alivyokuwa anavirusha kupitia chaneli yake ya Youtube ya Ngowi TV, inayohusu kliniki za ujasiriamali, alimtembelea fundi seremala, Festo Nyoni, aliyejiajiri kupitia kiwanda chake kidogo maeneo ya Mbezi Makabe.

Kama kawaida yake ya kutembelea wajasiriamali katika maeneo ya kufanyia kazi na kutoa elimu kidogo, mchumi huyo alitoa somo kwa mjasiriamali ili atengeneze faida anayostahili. Alimweleza kuwa faida inapatikana baada ya kutoa gharama zote za uendeshaji wa biashara ikiwamo ununuzi, usafiri, chakula. Alitoa mfano hai wa mlango ambao fundi huyo alikuwa akiutengeneza na kumweleza kuwa kinachopatikana baada ya kutoa gharama zote zilizotumika kutengeneza ndiyo faida.

Alimfundisha mjasiriamali huyo kutofanya kazi bila kujua gharama na faida atakayopata katika kila kazi atakayoifanya, na kwamba ni lazima awe na peni na karatasi kufanya mahesabu hayo.

Vile vile, alieleza anapochanganua gharama ni lazima aangalie kama vifaa anavyovitengeneza vinahitaji gharama ya jumla au ya kimoja, kama ni kifaa cha kufanyia marekebisho gharama zake zinaendana na marekebisho au ni bora atengeneze kifaa kipya.

Pia, ni muhimu mjasiriamali kujiwekea malengo ya faida katika kila bidhaa, kama ni asilimia 20 au 30. Kwamba ni lazima mjasiriamali ajisemee kuwa katika bidhaa hii ninayouza nataka nipate faida ya asilimia 25, hiyo itamsaidia mjasiriamali kuwekeza kwenye miradi mingine.

"Sasa kama fedha zote unazopata zinaishia kwenye material (vifaa vya ujenzi) mwisho wa siku hutokuwa na cha kuweka pembeni, ikizingatiwa kuwa unahitaji kuwekeza katika miradi mingine kwa kuwa kuna muda utafika hutokuwa na nguvu ya kubeba vitu vizito tena hivyo utahitaji biashara nyingine," alifafanua.

Alisema ili mtu aweze kuitumia faida na kuendeleza kipato ni lazima aipangie majukumu kabla hajaipata, ikiwamo kununua kiwanja au vifaa vya teknolojia ili kukuza ubora wa biashara.

Njia njingine ya kuitunza faida alisema kuwa ni kuwekeza katika taasisi za kifedha ikiwamo benki na Vikoba ili pia iwe rahisi kunufaika na mikopo kwa ajili ya kuendeleza biashara.

"Kuna utafiti tumefanya huko Pwani katika miji ya Kilwa, Rufiji, Mafya na sehemu mbalimbali katika familia za wavuvi na tumeona kuwa watu wanatengeneza hela kidogo, lakini hiyo hiyo wanaiwekeza kwenye Vikoba na wengi wamenunua viwanja, wamerekebisha nyumba kutokana na taratibu zilizopo za kukopa mara mbili au tatu," alifafanua Prof Ngowi.

Prof Ngowi alisema kuwa faida pia inaweza kutumiwa kwenye kukata bima ya afya ili kumpunguzia mjasiriamali gharama za ziada kujihudumia yeye pamoja na familia yake pale anapopata maradhi, lakini pia kujihakikishia uimara wa afya yake.


**TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA**
**P. O. Box 55, USA-RIVER, ARUSHA-MOSHI ROAD,**
**Tanzania, East Africa**

## JOB VACANCIES

Tumaini University Makumira (TUMA) invites qualified applicants to be considered for employment in the following teaching posts and their integrated Participatory and Integrative Teaching Approach (PITA) outreach programmes:

**1. Assistant Lecturers in Physics**

***Qualification:***
- A minimum GPA of 3.5 in Bachelor of Science (Physics) or Bachelor of Science with Education (Physics and other Science Subjects) or Bachelor of Education (Physics).
- A minimum GPA of 4.00 in Master of Science (Physics) or Master of Education (Physics)

**2. Assistant Lecturers in Chemistry**

***Qualification:***
- A minimum GPA of 3.5 in Bachelor of Science (Chemistry) or Bachelor of Science with Education (Chemistry and other Science Subjects) or Bachelor of Education (Chemistry).
- A minimum GPA of 4.00 in Master of Science (Chemistry) or Master of Education (Chemistry)

**3. Assistant Lecturers in Guidance and Counselling**

***Qualification:***
- A minimum GPA of 3.5 in Bachelor of Guidance and Counselling.
- A minimum GPA of 4.00 in Master of Guidance and Counselling.

**4. Assistant Lecturers in History**

***Qualification:***
- A minimum GPA of 3.5 in Bachelor of Arts with Education (History) or Bachelor of Education (History) or Bachelor of Arts (History)
- A minimum GPA of 4.00 in Master of Arts (History) or Master of Education (History)

***Job Descriptions & Duties***

Job descriptions and duties will be provided by respective departments after successful interviews and recruitment to the post.

Application letters with the attached CVs, copies of certificates and transcripts have to be sent before **Wednesday, 20th April 2022 to:**

**THE VICE CHANCELLOR,**
**TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA,**
**ARUSHA-MOSHI ROAD,**
**P. O. Box 55, USA-RIVER.**

**OR VIA EMAIL:**
**vc@makumira.ac.tz**
**(Attachments of CV, copies of Certificates and Transcripts should not exceed 10 MB)**

216797002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji Simba sasa wajifunze kunufaika na VAR michuano Caf

**SHIRIKISHO** la Soka Afrika (CAF), limetangaza kuanzia hatua ya robo fainali na kuendelea kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu, teknolojia ya video maalum kwa ajili ya kumsaidia mwamuzi (VAR), itaanza kutumika rasmi.

Hii itakuwa mara ya kwanza katika historia ya soka la nchi hii na Afrika Mashariki, VAR kutumika katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini pia kwa Wawakilishi wa Tanzania, Simba kuwa klabu ya kwanza nchini kutumia teknolojia hiyo kwenye mashindano hayo ya Afrika.

Simba kama zilivyo klabu nyingine katika mashindano hayo ya CAF, itaanza kutumia VAR kwenye mechi yake ya kwanza ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho itakapoikaribisha Orlando Pirates ya Afrika Kusini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii.

Simba ambao ni wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye mashindano ya kimataifa ngazi ya klabu, itahitaji kushinda kwa idadi kubwa ya mabao kwenye mechi hiyo ili kurahisisha kazi ya kufuzu nusu fainali watakaporudiana ugenini wiki moja baadaye.

Tunaamini hilo linawezekana hasa kutokana na uwezo wa kikosi cha Simba pamoja na benchi lao la ufundi, lakini wakipata nguvu kubwa kutoka kwa mashabiki 60,000 walioruhusiwa kuingia uwanjani, hivyo kilichobaki ni wachezaji kuelekezwa tu namna ya kunufaika na VAR katika mchezo huo.

Hata hivyo, kwa kasi ya mawinga wa Simba, Bernard Morrison na Pape Sakho, ambao mara nyingi hukokota mpira na kulazimisha kuingia nao ndani ya 18, tunaamini VAR inaweza kuwa upande wao kwa kunufaika na penalti endapo wachezaji hao wakielimishwa kucheza na akili ya mwamuzi lakini pia namna ya kugongana kwa faida.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba mara nyingi mwamuzi hulazimika kwenda kuangalia marudio ya tukio husika kwenye VAR endapo tu wachezaji watamfuata kulalamika kutoridhishwa na uamuzi alioutoa kuhusu faulo ama madhambi yoyote watakayotendewa.

Kama wachezaji wa Simba watachukulia 'poa tu' (sawa tu) kwa kila uamuzi ambao mwamuzi anatoa dhidi yao bila kumfuata kulalamika, ni wazi hawatanufaika na VAR, hivyo kuwanufaisha wapinzani wao, Orlando Pirates.

Lakini pia wachezaji wa Simba hawana budi kuwa makini kwa kuepuka kucheza madhambi hususan ndani ya eneo la hatari kwani wapinzani wao nao watakuwa makini wakitaka kunufaika na VAR, ambayo inang'ata pande zote.

Kwa mantiki hiyo, benchi la ufundi linapaswa kuwakumbusha na kusisitiza namna ya kunufaika na VAR, kwani tunaamini wachezaji nao wamekuwa wakifuatilia mechi mbalimbali ambazo teknolojia hiyo imekuwa ikitumika, na kuona namna gani wenzao wanafanya ili kumshawishi mwamuzi kwenda kujiridhisha.


Katika hilo pia, ni wakati muafaka kwa wachezaji wa klabu zote nchini kuanza kujifunza mengi kupitia mechi hiyo na nyinginezo, kuhusu namna ya kunufaika na VAR.

Tunasema hivyo, kutokana na ukweli kwamba, ni wazi mafanikio ya VAR katika hatua hii ya robo fainali msimu huu, yanaweza kuchochea CAF kutangaza teknolojia hiyo kuanza kutumika kwenye michuano yake yote kuanzia hatua za awali msimu ujao.

Pamoja na hayo yote, benchi la ufundi la Simba wanapaswa kusoma na kuchanga vema karata zao kwa kuandaa mbinu zitakazowalazimisha wapinzani wao kucheza madhambi zaidi kwenye mechi hiyo na hata ile ya marudiano ugenini.

Lakini pia, Simba haina budi kufanya maandalizi ya kutosha kuelekea mchezo huo ambao tunaamini utakuwa mgumu kwa kila upande hasa kwa wawakilishi hao wa Tanzania ambao watakuwa na presha kubwa ya kutaka kupata ushindi nyumbani. Kila Kheri Simba katika maandalizi ya mechi hiyo muhimu kwenu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba itumieni vema 'nyomi' ya mashabiki 60,000 kwa Mkapa

Na Adam Fungamwango

KWA mara ya kwanza kwenye historia ya soka la Tanzania, teknolojia ya kumsaidia mwamuzi (VAR) itatumika nchini kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba itakapoivaa Orlando Pirates kutoka Afrika Kusini, Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ni baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuamua mechi zote za robo fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, kutumia teknolojia hiyo ili kuongeza ufanisi kwenye maamuzi.

Pia, CAF ikakubali ombi la klabu ya Simba kuingiza mashabiki 60,000 kwenye mechi hiyo, ikiwa na maana wamekubali uwanja mzima ujae, kwani Uwanja wa Benjamin Mkapa, unaingiza idadi hiyo ya mashabiki.

Hii ina maana kuwa mechi hiyo inayotarajiwa kucheza saa 1:00 usiku, itarudisha kumbukumbu zilizowahi kupita za Ligi ya Mabingwa Afrika ilivyoingiza idadi hiyo ya mashabiki ambao walikuwa wamejaa uwanja mzima na kuufanya kurindima kwa kushangilia, kelele, na ngoma ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa zikiwachanganya wapinzani.

Mechi hizo ni dhidi ya Nkana FC ya Zambia, ambapo 'nyomi' la mashabiki lilichangia kwa kiasi kikubwa Simba kupata ushindi wa mabao 3-1 na kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa, Desemba 23, 2018, wakati ilikuwa imetoka kufungwa mabao 2-1 nchini Zambia.

Machi 16, 2019, umati mkubwa wa mashabiki wa Simba uliojaa Uwanja wa Benjamin Mkapa, uliwasukuma wachezaji wa timu hiyo kupambana na kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya AS Vita Club kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, ikatinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo. Ugonjwa wa UVIKO-19, ndiyo uliopunguza mashabiki uwanjani kwani msimu uliofuata Simba pamoja na kufika robo fainali, lakini haikuwa na mashamsham kama yale ya msimu wa kwanza, kwa sababu kuna wakati iliruhusiwa kuwa na mashabiki 15,000, 20,000 mpaka 35,000. Kuna baadhi ya mechi hazikuwa kabisa na mashabiki, ukiwamo dhidi ya Al Merrikh ya Sudan uliochezwa Machi 16, 2021.

Klabu ya Simba, pamoja na kwamba imesajili timu nzuri kwa miaka ya karibuni na kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa, lakini sapoti kubwa imekuwa ni kutoka kwa mashabiki wake kama mchezaji wa 12 ambao kwa sasa wamekuwa maarufu sana Afrika kwa ushangiliaji wao, unaovutia na kuzitisha timu nyingi na makocha wengi.

Mmoja wapo ni Kocha wa Al Ahly ya Misri, Pitso Mosimane, ambaye alikutana na joto ya jiwe wakati timu yake ilipochapwa bao 1-0 nchini kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Februari 23, mwaka jana.

Moja sababu ya kupoteza, aliwataja mashabiki wa Simba kuwa washangilia kwa nguvu mno na kuwafanya wachezaji wao kupambana. Na hata hivyo kwenye mechi hiyo CAF waliruhusu mashabiki 25,000 tu.

Pitso, mara kwa mara, hata kwenye droo ya CAF, amekuwa akizitahadharisha timu zinazokwenda kucheza Benjamin Mkapa, kutokana na aina ya mashabiki wake jinsi wanavyoshangilia.

Kutokana na hilo, ni kwamba wachezaji wanatakiwa kuwatumia mashabiki 60,000 watakaokuwa nyuma yao kwa ajili ya kupata ushindi mnono, ili kazi iwe rahisi kama ya kumsukuma mlevi Sauzi.

Kingine ni jinsi ya kuitumia VAR. Bernard Morrison anaweza kuwa msaada mkubwa kama akipata mpira huwa harudi nyuma. Ndiye mchezaji pekee anayeweza kukokota mpira akiwafungasha tela mabeki, akiingia kwenye eneo la penalti. Anachotakiwa kufanya hivyo hivyo, kuingia nao tu kwenye eneo la hatari ili kama akiangushwa basi kuna uwezekano mkubwa wa kupata penalti hata mbili kwa aina ya uchezaji wake.

Lakini pia wachezaji wa Simba wanatakiwa wawe walalamishi pale mchezaji wao anapoangushwa ndani ya eneo la hatari ili kumshawishi mwamuzi kwenda kuangalia kwenye VAR, kwani la sivyo anakuwa hana ulazima huo kwa sababu hakuna aliyelalamika. Lakini nao wanatakiwa wapunguze makosa yasiyo ya lazima langoni mwao.

# Mbaroni kwa tuhuma za ujangili

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wawili wakazi wa Kijiji cha Matandu, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, wanashikiliwa kwa mahojiano na Polisi kwa tuhuma za kujihusisha kumiliki silaha na uwindaji haramu wa nyara za mbalimbali za Serikali.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, aliwataja wanaoshikiliwa ni Omari Abdulrahman Mpamba na Hemedi Nassoro Malowa, wote wakazi wa Kijiji cha Matandu, Wilaya ya Kilwa.

Kitinkwi alisema watuhumiwa walikamatwa mwishoni mwa wiki majira ya mchana katika msako uliofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na askari wa wanyamapori wa kwenye Pori la Akiba Selous kusaka watu wanaojihusisha na uwindaji haramu wa nyara za serikali.

Alisema katika msako huo walikamata bunduki moja aina ya S/Gun Greener namba 36452, risasi (13), maganda yakiwamo ya bunduki aina ya Riffle yaliyotumika (26) bila kuwa na kibali.

Kitinkwi alifafanua kuwa Omari Abdulrahman Mpamba alikutwa na bunduki hiyo pamoja na risasi sita, maganda mawili yaliyotumika, huku akidai alikuwa ameazimishwa na Hemedi Nassoro Malowa, kwa ajili ya kufanyia uwindaji haramu wa wanyamapori.

Kamanda huyo alisema baada ya mahojiano askari walikwenda nyumbani kwa Malowa na kufanya upekuzi na kukutwa akiwa na risasi saba za bunduki aina ya Riffle, maganda 22 yaliyotumika na maganda mawili ya S/Gun na golori 204 kubwa tatu na ndogo 201.

Pia alisema katika upekuzi huo nyumbani kwa Malowa walikamata mtambo wa kutengenezea pombe aina ya gongo.

Alisema upelelezi unaendelea kubaini mtandao unaojihusisha na uwindaji haramu, na kwamba baadaye watuhumiwa watafikishwa mahakamani.




Mkuu wa Wilaya ya Serengeti Dk. Vicent Mashinji (wa pili kulia) akipokea mabati 118, mbao 400, misumari kilo 80 na waya za kufungia kenchi kutoka kwa Meneja wa Kanda wa NMB Baraka Stanslaus, kwa ajili ya kuezekea madarasa mawili ya Shule ya Msingi Bwitengi katika wilaya hiyo mkoani Mara, kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo Anthony Guzuye na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Kamara (kulia) wakishuhudia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali wanawake wahakikishiwa soko la nje

**Na Mwandishi Wetu,** BERLIN UJERUMANI

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, amesema Wizara yake itashirikiana na balozi zilizopo katika nchi mbalimbali duniani kutumia fursa zilizopo katika nchi hizo ikiwamo masoko kwa ajili ya bidhaa za wajasiriamali wanawake kutoka Tanzania.

Dk. Gwajima alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini Berlin nchini Ujerumani, baada ya kumalizika kwa Mkutano wa G7 uliokwenda kuwawezesha wajasiriamali hasa wanawake katika kuendeleza biashara zao kwa kupata masoko ya Kimataifa.

Dk. Gwajima aliwapongeza kinamama kutoka Tanzania walioshiriki kwenye maonyesho ya bidhaa za mboga na matunda, na kuwaomba kuwashirikisha wanawake wengine wa Tanzania kwa lengo la kupanua wigo wa upatikanaji wa masoko ya bidhaa hasa masoko ya kimataifa.

Alimpongeza Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Abdallah Posi, kwa maandalizi mazuri na mapokezi mazuri waliyoyapata wakati wa Mkutano wa G7.

"Tunamshukuru sana Balozi Posi kwa maandalizi mazuri ambayo yamefanywa, lakini pia tunampongeza Balozi Hoyce Temu aliyesafiri kutoka Uswisi hadi hapa Berlin kuja kuungana na wajasiriamali kutoka Tanzania walikuwa na kampuni zaidi ya 12, hakika hili limeongeza nguvu na umuhimu wa Mkutano huu kwa Ustawi wa Wajasiriamali Tanzania," alisema Dk. Gwajima

Alisisitiza kuwa Wizara kwa kushirikiana na balozi mbalimbali kote duniani itahakikisha inashirikiana ili fursa za masoko na zingine zilizopo ziweze kuwafikia wanawake wa Tanzania na jamii kwa ujumla.

"Tumejifunza na kuona fursa zilizopo huku Ujerumani na nchi zingine zote zinashirikiana na Tanzania kupitia ubalozi wetu na niahidi kutumia tuliyojifunza kutokana na mkutano huu wa G7 kwa Wanawake wa Tanzania na jamii kwa ujumla" alisema.

Akiwa katika Mkutano wa G7 alitembelea mabanda ya Watanzania wakiwa kwenye maonyesho ya Berlin Messe nchini Ujerumani ambayo yalishirikisha wafanyabiashara wa mazao ya kilimo kutoka Arusha, Njombe na Iringa.

# SWAUTA yaomba Serikali kuanzishwa kwa shule maalumu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WANAWAKE wenye ulemavu Mkoa wa Pwani wameiomba serikali ya mkoani humo kuanzisha shule maalumu ya sekondari kwa ajili ya watoto wenye ulemavu wa kusikia, kuona na wenye ualbino ambao kwa sasa wanalazimika kusoma nje ya mkoa huo.

Ombi hilo limetolewa juzi mjini hapa na Sauti ya Wanawake wenye Ulemavu mkoa wa Pwani (SWAUTA), walipokuwa wakishiriki semina ya siku moja iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa wanawake wenye ulemavu wa Wilaya ya Kibaha.

Katika risala yao waliyoisoma kwa mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Pwani ambaye ni Mganga Mkuu wa mkoa, Gunini Kamba, walisema kwa sasa watoto wenye ulemavu wanaohitimu elimu ya msingi wanalazimika kwenda kupata elimu ya sekondari katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Iringa.

SWAUTA ilisema kukosekana kwa shule ya sekondari kwa watoto wenye mahitaji maalumu kunasababisha baadhi yao kushindwa kuendelea na masomo na kuishia elimu ya darasa la saba.

Pia, walielezea kikwazo kingine wanachokutana nacho kuwa ni ukosefu wa wenye ulemavu kwenye sehemu za kutolea huduma na kwenye vikao na kusababisha wanawake kushindwa kushiriki kikamilifu.

Dk. Gunini alisema vikwazo vilivyoainishwa na SWAUTA atavifikisha kwa Mkuu wa mkoa kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

Mwenyekiti wa SWAUTA, mkoa wa Pwani, Tatu Kondo alisema wamepata semina hiyo baada ya kupeleka maombi EWURA, wakiomba kupatiwa elimu ya shughuli zinazofanywa na Mamlaka hiyo.

Aliwashukuru EWURA kwa kutekeleza maombi hayo na kundi hilo lililowakilishwa na watu 80 lilinufaika na elimu hiyo.

Naye Meneja EWURA wa Kanda ya Mashariki, Nyirabu Musira, alisema wametoa elimu ya shughuli zinazofanywa na mamlaka hiyo kwa kundi hilo kwakuwa ni watu ambao hawafikiwi mara kwa mara.

Ofisa Mkuu wa Huduma kwa wateja wa EWURA, Michael Mshighwa, akitoa mada, aliwaeleza washiriki kuwa uchakavu wa miundombinu ya umeme na maji ni moja ya sababu za ongezeko la bili kama haikugundulika na kukarabatiwa kwa wakati.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Afrika, Nehemia Mchechu akiongea na viongozi wa benki hiyo wakati alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi za makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam juzi, (wa kwanza kushoto) ni Mkurugenzi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo, Adam Mihayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanri awapa mbinu wakulima wa pamba

**Na Idda Mushi,** KILOSA

BALOZI wa Pamba nchini, Agrey Mwanri, amewataka wakulima kuchukua hatua kukabiliana na uvamizi wa wadudu waharibifu wa zao hilo hasa kwa kuzingatia matumizi sahihi ya pembejeo ikiwemo viuatilifu.

Mwanri pia ametoa msamaha wa kipindi hiki cha Kwaresma na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa watu waliojichukulia viuatilifu bila kuwa na mashamba kurejesha mara moja bila masharti yoyote kabla ya kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Mwanri alitoa ushauri huo katika vijiji mbalimbali vya wilaya ya Kilosa, wakati akitoa elimu sahihi ya upuliziaji viuatilifu kukabiliana na wadudu waharibifu wa zao la pamba wakiwamo chawa jani, kidung'ata, kanga mbili na funza. "Baadhi mmechukua dawa (viuatilifu) wakati hamna mashamba, mnaishia kuuza au kwenda kutumia kwa mazao mengine, jambo ambalo ni hatari sana kiafya... hii ni sumu kali na inaua, haifai kwa mazao ya mboga wala mazao ya chakula, rudisheni wapewe wakulima waliolima pamba," alisema.

Mwanri alisisitiza afya ya binadamu ni muhimu zaidi kuliko zao la pamba, na bila kuwa na watu wenye afya njema, ni ngumu kulima pamba wala kufanya maendeleo yeyote, hivyo aliwahimiza wananchi kuzingatia afya zao wakati wa kilimo cha pamba.

Aidha, aliwaonya kuacha kukoroga sumu na kupulizia juu juu kienyeji, kwani kwa kufanya hivyo hawataweza kuwaua wadudu wanaoshambulia kwa kasi pamba, na ambao wamesambaa maeneo yote nchini, badala yake akawaelekeza namna sahihi ya kuchanganya dawa na kupulizia juu na chini ya mimea kwa kutumia kifaa aina ya solo.

Ofisa Tarafa wa tarafa ya Ulaya wilayani Kilosa, Halima Nyange, alishukuru kwa elimu iliyotolewa na tahadhari za kiafya zikiwemo kutumia mifuko ya nailoni kuziba mikono, kuvaa barakoa wakati wa kupulizia sumu shambani na nguo za kufunika miguu na mikono wakati wa shughuli za shamba ili kuepuka madhara ya kiafya ambayo wakati mwingine hayaji papo hapo bali huchukua muda.

Wanunuzi wa pamba kanda ya mashariki kupitia Mkurugenzi wa Kampuni ya Upami Agrobusiness LTD, Johnson Lipagila, aliahidi kuendelea kuwapatia zaidi wakulima pembejeo na elimu ili kuongeza uzalishaji wa pamba kuwa wenye tija na ubora kimataifa.

# Uhamiaji yawapa masharti wageni kufanya kazi mashamba ya tumbaku

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAKULIMA wa tumbaku katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wanaoajiri vibarua kutoka nje ya nchi wametakiwa kuwakatia vibali vya kufanyia kazi.

Idara ya Uhamiaji imeanzisha utaratibu wa kutoa vibali vya muda vya kufanya kazi nchini vya kuanzia miezi mitatu na kuendelea kwa raia wa kigeni mradi asiwe na umri wa chini ya miaka 18 ili kuepuka kukamatwa.

Baadhi ya wakulima wa tumbaku hasa katika Halmashauri ya Ushetu walikuwa wakiajiri watoto umri wa miaka 18 na kuwafanyisha kazi katika mashamba na wengine kuchunga mifugo, lakini kuanzia sasa ni marufuku.

Maelekezo hayo yalitolewa juzi na Ofisa Uhamiaji Wilaya ya Kahama, Salumu Rashid, na kuongeza kwamba wamiliki wa mashamba ya tumbaku wakiwakatia vibali raia wa kigeni, kutapunguza adha ya kukamatwa mara kwa mara, kwa kuwa watakuwa wamefuata utaratibu.

Rashidi alisema kama wakulima hao watakuwa wakitaka vijana kwa ajili ya kuchunga mifugo na kufanya kazi katika mashamba ya tumbaku, ni bora wakafuata sheria ya kuwakatia vibali vya muda kwa ajili ya kuishi nchini, na kuongeza kuwa gharama zake ni Sh. 50,000.

Alisema kwa atakayefuata utaratibu hatakamatwa na kuongeza kuwa hata serikali itakuwa ikiingiza mapato mengi kupitia vibali hivyo.

# Dirisha lafunguliwa rasmi kidato cha nne kubadili tahasusi

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imetoa fursa kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha nne mwaka 2021 kufanya madadiliko ya machaguo au tahasusi (combination), kozi mbalimbali wanazohitaji kusoma kulingana na ufaulu wao ikiwa ni mwaka wa nne sasa tangu kuanza mpango huo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa alisema hatua hiyo inatokana na baadhi ya wanafunzi waliohitimu kutokujaza fomu (Selform) kwa uhakika wakati wanachagua 'combination' (mchepuo) zao kutokana na kutokuwa na uhakika wa ufaulu katika masomo yao.

"Fursa hii huwawezesha wanafunzi kubadilisha machaguo kulingana na ufaulu walioupata kwenye matokeo ya mtihani wa kidato cha nne wa mwaka 2021 yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)," alisema Bashungwa

Alisema kutokana na ufaulu huo Ofisi ya Rais- TAMISEMI inatoa fursa kwa wahitimu hao kubadili machaguo yao, ili kutoa mwanya zaidi kwa mwanafunzi kusoma tahasusi itakayomuandaa kuwa na utaalamu fulani katika maisha yake ya baadaye kwa namna ambayo anatamani.

Aidha, alitoa rai kwa wazazi kushirikiana na watoto wao katika suala hilo, ili baada ya uchaguzi wa kombinesheni hizo kufanyika kusiwapo na malalamiko yoyote kuhusu mtoto kupangiwa machaguo ambayo hakupangiwa.

"Ofisi ya Rais -TAMISEMI imekamilisha zoezi la awali la kuingiza kwenye kanzi data taarifa zilizo kwenye fomu za mwanafunzi kama zilivyojazwa na wanafunzi wakiwa shuleni, hii inatoa nafasi kwa wanafunzi kuweza kufanya mabadiliko ya machaguo yao kadiri watakavyoshauriwa kwa njia ya mtandao, "alisema Bashungwa

Bashungwa aliendelea kufafanua kuwa baada ya wanafunzi kufanya marekebisho yao kanzi data hizo ndizo zitakazotumika kuwachagua na kuwapangia nafasi za kidato cha tano na kozi mbalimbali katika vyuo vya kati.

Aliwakumbusha wanafunzi wanaopenda kufanya mabadiliko ya tahasusi zao kuingia kwenye mfumo wa uchaguzi wa wanafunzi (student selection, MIS) unaopatikana kupitia kwenye kiunganishi cha selform. tamisemi.go.tz. Alisema kuwa serikali imetoa fursa kwa wahitimu wa kidato cha nne kubadili machaguo yao, ili kutoa nafasi zaidi kwa mwanafunzi kusoma tahasusi au kozi itakayomwandaa kuwa na utaalam ambao unaendana na machaguo yake hapo baadae.

Aliwakumbusha wanafunzi kuzingatia muda uliotolewa wa kufanya marekebisho hayo ambao ni kuanzia Machi 30 hadi Aprili 19,2022, ili ratiba ya kuwachagua na kuwapangia shule iende kwa muda uliopangwa.

"Huduma hii ya kubadilisha tahasusi ni bure na endapo mwanafunzi atapata changamoto awasiliane na huduma kwa wateja kupitia baruapepe helpdesk@tamisemi.go.tz," alisema.

# Dodoma kukamilisha mfumo anwani za makazi kwa wakati

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru amewataka wasimamizi wa mradi wa uwekaji wa mfumo wa anwani za makazi kukamilisha kwa wakati. Mafuru alitoa agizo hilo juzi baada ya kukabidhiwa kibao cha anwani ya makazi kutoka kwa Mratibu wa mradi huo kwa ajili ya mtaa wa CDA jijini Dodoma.

Alisema wasimamizi wa mfumo huo wanatakiwa kukamilisha kabla ya Aprili 15, mwaka huu na inatakiwa mitaa yote iwe imewekwa na kuzifunga anwani hizo. "Ni mategemeo yangu kuona maeneo yote ya mitaa imewekwa kabla ya tarehe tuliyojiwekea ya Aprili 15, mwaka huu iwe imefungwa anwani hizo ili muweze kukamilisha malengo yenu," alisema.

Mratibu wa mradi huo wa uwekaji wa mfumo wa anwani za makazi Jiji la Dodoma, Joseph Nkuba, alisema mpaka sasa jumla ya kata 38 kati ya 41 zimeshawekwa nguzo na vibao.

Alisema kuwa kutokana na juhudi kubwa za ufanisi wa uwekaji wa anwani hizo watafanikiwa kuifanya Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuwa ya kwanza kukamilisha kazi hiyo.

"Zoezi hili lilianza Machi 15, 2022, mpaka sasa tumefikia kata 38 bado tatu kuzifikia, hivyo kwa asilimia 60 tuna uhakika tunaenda kumaliza na kuifanya halmashauri yetu ya Dodoma kuwa ya kwanza kati ya halmashauri zote nchini," alisema.

"Nitoe rai kwa watendaji wa kata, mitaa, wadau wa maendeleo na wenyeviti wa mitaa kushiriki kwa ukamilifu na wasimamizi wake ili zoezi hilo likamilike kwa wakati,"alisema.

Aliziomba taasisi za watu binafsi na serikali kushiriki katika kuchangia gharama za nguzo na vibao ili kufungwa na kukamilisha kwa wakati.




Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Joyce Mayanja akizindua kisima cha maji safi na salama kilichofadhiliwa na kampuni ya bia ya Serengeti (SBL) na kujengwa na shirika la maji la WaterAid, wilayani humo, mkoani Manyara jana. Nyuma yake ni Mkurugenzi Mkazi wa WaterAid, Anna Mzinga (mwenye miwani), kulia kwake ni Mkurugenzi wa Mawasiliano ya SBL, John Wanyancha, kulia kwake akifuatiwa na Kaimu Mkurugenzi wa Ruwasa Mkama Bwire na mbele yake akiwa ni Mwenyekiti wa Halmashauri wilaya ya Hanang, Rose Kamili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunifu watakiwa kuangalia mahitaji ya Afrika

**Na Joseph Mwendapole**

WABUNIFU nchini wameshauriwa kuangalia mahitaji ya nchi za Afrika wanapofanya ubunifu wao ili waweze kupata mapato makubwa badala ya kuangalia mahitaji ya hapa nchini pekee.

Meneja wa Kitengo cha Ubunifu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Athumani Mgumia, ndiye aliyetoa ushauri huo wakati wa mashindano ya ubunifu kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Mashindano hayo yaliyofanyika kwenye maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), yaliwashirikisha wanafunzi 10 kwa lengo la kupata washindi wawili wa Tanzania.

Washindi hao wawili watakwenda kuchuana na wenzao nane kutoka nchi za EAC kwa lengo la kupata mshindi wa jumla atakayejinyakulia Dola za Marekani 10,000 na yamedhaminiwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ).

Mgumia alisema COSTECH imeshafungua milango kwa nchi mbalimbali ambapo wabunifu kutoka Tanzania wanaweza kushiriki na kujipatia kipato kwa kuwasilisha ubunifu wa kutatua changamoto mbalimbali.

"Milango imeshafunguka kwa hiyo wanapofanya ubunifu wasiangalie mahitaji ya hapa ndani tu waangalie mahitaji ya mataifa ya Afrika ili waweze kupata soko kubwa la bidhaa zao na hatimaye kujiongezea mapato," alisema.

Alisema nchi za Afrika zina matatizo mengi ambayo wabunifu hao wanaweza kuyatumia na kuja na suluhisho lake kwa kubuni mbinu za kuyatatua na wao kutumia fursa hiyo kuinua vipato vyao.

"Kwa mfano wananchi wengi wanaishi maeneo ya vijijini ambako shughuli kubwa ni kilimo sasa wabunifu wanaweza kubuni vitu vya kusaidia uzalishaji kuwapunguzia gharama wakulima wetu na wao kunufaika na bunifu hizo," alisema

Mgumia alisema (COSTECH) inawapongeza waandaaji wa mashindano hayo kwani yatasaidia kuibua vipaji mbalimbali kwa vijana ambao watajiajiri na kupunguza tatizo la ajira.

Aliwapongeza waandaji kwa kuwapa mafunzo washindani wabunifu wa hapa nchini kabla ya kushiriki mashindano hayo kwani yatawapa uzoefu wa kushiriki mashindano mengine.

Alisema vijana walioshiriki kwenye mafunzo hayo wamejengewa uwezo wa namna ya kuendeleza ubunifu wao na namna ya kushiriki kwenye mashindano mengine yatakapokuja.

Mratibu wa mashindano hayo, Abdulkarim Bihaki kutoka GIZ, alisema lengo la mashindano hayo ni kuhakikisha vijana wanapata ujuzi unaohitajika kwaajili ya kujiajiri wanapomaliza mafunzo badala ya kuhangaikia ajira.

Alisema mradi huo unawashirikisha mbalimbali katika utekelezaji wake kama Baraza la Vyuo vya Afrika Mashariki ambalo linafanya kazi na vyuo mbalimbali katika nchi hizo.

"Wiki tatu zilizopita tulifanya Uganda, Sudani Kusini, Rwanda na tukaenda Kenya na wiki hii tunafanya Tanzania na Burundi, kwenye mashindano haya vijana wanakuja na mawazo ya namna wanavyoweza kutatua changamoto kwenye jamii yetu na tunayaendeleza," alisema

Alisema washindi wawili kutoka Tanzania watashindana na wengine nane watakaotoka nchi hizo sita za Afrika Mashariki ambapo mshindi wa jumla atajinyakulia Dola za Marekani 10,000.

Alisema washindi wawili wa Tanzania watazawadiwa Dola za Marekani 1,500 na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kabla ya kwenda kushindana na wenzao wa Afrika Mashariki.

## Shule Serengeti yasaidiwa mabati

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Msingi Bwitengi Kata ya Manchira Wilaya ya Serengeti mkoani Mara imepokea msaada wa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 8.

Vifaa hivyo vilitolewa na Benki ya NMB kupitia mpango wake wa kuwajibika kwa jamii.

Akizungumza katika hafla fupi ya makabadhiano iliyofanyika katika Shule ya Msingi Bwitengi, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, alisema wataendelea kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ya Serengeti katika shughuli za maendeleo.

"Tulipopata maombi kutoka shule hii, sisi kama NMB tukaona ni vyema tukawasaidia na leo tumeweza kuwaletea mabati 118, mbao 400, Kilogramu 80 za misumari na waya za kushikia kenchi Kilogramu 16," alisema Ladislaus na kuongeza kuwa wataendelea kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya 6 ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Benki yetu itaendelea kuinua sekta ya elimu na kwa mwaka huu, tutaanza ufadhili kwa wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na chuo kikuu, lakini wakishindwa kwa sababu za kiuchumi. Benki ya NMB itawagharamia ada, malazi pamoja na kuwapa vitendea kazi kama kompyuta kuwasaidia masomoni," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Dk Vicent Mashinji, ameipongeza benki hiyo kwa kutoa msaada huo na kuwaomba wakazi wa kijiji cha Bwitengi na wana Serengeti kwa ujumla kuendelea kushirikiana vyema kwa maendeleo ya wilaya ya Serengeti.

Mkuu wa Shule ya Msingi Bwitengi, Melau Mollel, aliishukuru benki hiyo kwa kuisaidia shule yao, huku akiwaomba wasichoke kuisaidia shule yao kwani bado wana mahitaji mengi, yakiwamo mashimo 32 ya vyoo ili kukidhi idadi kubwa ya wanafunzi waliyo nayo.

Alisema wanakabiliwa na uhaba wa nyumba 18 za walimu, ofisi tatu za walimu na madawati 266.

# Kafulila awafagilia waganga tiba asili

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amesema serikali inatambua mchango wa waganga wa tiba asilia na tiba mbadala katika sekta ya elimu mkoani humo.

Kafulila alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza katika kongamano la waganga mjini Bariadi na kuhudhuriwa na waganga kutoka wilaya zote za mkoa huo.

Alisema mafanikio ya mkoa huo katika sekta ya elimu yamechangiwa na wadau mbalimbali na waganga hao ni sehemu hiyo kwani wamefanya kazi ya kutoa michango mbalimbali .

Alisema waganga hao wamekuwa mstari wa mbele katika kufanikisha kuwapo kwa kambi ya kitaaluma kwa wanafunzi waliopo kwenye madarasa ya mitihani yakiwamo darasa la nne,darasa la saba, kidato cha nne na cha sita.

Alisema wamekuwa wakitoa michango kwa ajili ya kuwapatia motisha chanya walimu wa shule za msingi na sekondari waliofanya vizuri katika kufundisha masomo yao katika mitihani ya kitaifa sambamba na kuwapa motisha wanafunzi waliofanya vizuri kwenye mitihani yao ya kitaifa.

Kafulila aliongeza kuwa mara baada ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa mkoa huo mwaka 2020 alikuta ukiwa na nafasi ya tano kwa matokeo ya kidato cha nne lakini kwa matokeo ya mwaka 2021 yaliyotangazwa mwaka huu kwa kidato hicho umeshika nafasi ya tatu hivyo wanajipanga kushika nafasi ya juu yaani namba moja mwaka huu.

"Michango hii mnayoitoa katika sekta ya elimu hizi salamu zenu zinafika kwa viongozi wa ngazi za juu wa serikali ambao ni Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu na wakuzipeleka ni mimi mkuu wenu wa mkoa," alisema Kafulila.

Alifafanua kuwa kutokana na matokeo hayo mazuri ya mwaka jana katika kuwapatia motisha walimu na wanafunzi waliofanya vizuri watatoa zawadi zenye thamani ya Sh milioni 81.

Aidha, katika kutambua mchango wa waganga hao katika sekta hiyo, Kafulila alikabidhi vyeti vya kutambua mchango huo kwa waganga hao katika wilaya za mkoa huo ambazo ni Maswa, Bariadi, Itilima, Busega na Meatu.

Awali, mlezi wa waganga hao Mkoa wa Simiyu, Shemsha Mohamed ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Simiyu alimkabidhi Mkuu wa mkoa huo, mchango wa ng'ombe 13 na mbuzi 53 zilizotolewa na waganga hao kwa hiari yao kuunga mkono jitihada za mkoa huo katika sekta ya elimu ikiwa ni sehemu ya kuchangia motisha kwa walimu na wanafunzi.

Naye Mwenyekiti wa waganga hao katika mkoa huo, Dk. Shija Limbe alisema kuwa michango yote wanayoitoa katika shughuli za maendeleo ikiwemo hiyo ya elimu inatolewa kwa hiari yao bila kulazimishwa na mtu yeyote.

Alikabidhi Sh 1,420,000 zilizochangwa na waganga hao katika kongamano hilo huku ahadi zikiwa Sh 300,000 kiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za uongozi wa mkoa huo katika sekta ya elimu. "Hii michango tunayochangia katika shughuli za maendeleo katika mkoa wetu hususan sekta ya elimu tunaitoa kwa hiari yetu na hii mifugo na fedha hatujalazimishwa na mtu maana kuna maneno maneno yanasemwa tumelazimishwa ni uongo na hatuwezi kukatishwa tamaa sisi tunajitambua maana elimu inawagusa watoto wetu," alisema

# Wenye ulemavu wapewa msaada wa mil. 40/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MGODI wa dhahabu wa Bulyanhulu, Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, umetoa msaada wa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 40 kwa wazee na watu wenye ulemavu 210 wanaotoka katika vijiji vinavyozunguka mgodi huo.

Msaada huo ni baiskeli 30, vifaa vya kusikia vitano, fimbo nyeupe sita, vyerehani, televisheni na pikipiki kwa ajili ya dawati la jinsia Bugarama ili kusaidia kupambana na ukatili wa kijinsia.

Akikabidhi msaada huo jana, Meneja Uhusiano na mazingira wa mgodi huo, Agapiti Paul, kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga alisema, wataendelea kuwasaidia wazee na watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kushiriki shughuli za kiuchumi.

Paul alisema, fedha za ununuzi wa vifaa hivyo ni sehemu ya Sh.bilioni 2.5 zilizotengwa na mgodi huo kwa ajili ya miradi ya uwajibikaji wa jamii (CSR) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 katika Halmashauri ya Msalala.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, aliupongeza mgodi huo kwa kuona umuhimu na kuwapatia wazee na watu wenye ulemavu vitendea kazi ambavyo vitawasaidia kuondokana na utegemezi katika jamii.

Alisema wakati serikali ikielekea katika uchumi wa kati ni vyema kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na msaada huo anategemea kuona unawanufaisha watu wote wenye ulemavu na wazee.

Vile vile, Kiswaga alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Charles Fussi, kuvitambua vikundi vyote vya watu wenye ulemavu na kuvisajili kwa kuvipatia mikopo isiyokuwa na riba ili kuinua mitaji yao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, aliwataka watu wenye ulemavu kujitokeza kupata mikopo isiyokuwa na riba inayotolewa na halmashauri hiyo na kabla ya kupata ni vyema wakapata elimu ya miradi wanayotekeleza ili wainuke kiuchumi kwa haraka zaidi.

Alisema, mwaka huu wa fedha halmashauri hiyo imetoa Sh. milioni 300 katika vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, na bado kuna zaidi ya Sh. milioni 100 na kuwataka kuunda vikundi kupitia ofisi za maendeleo ya jamii kata ili kuchangamkia fursa hiyo.

Mwenyekiti wa kikundi cha wenye ulemavu Kata ya Bulyanhulu, Abbas Hassan, aliushukuru mgodi huo kwa kuwathamini na kuwajali watu wenye ulemavu kwa kuwapatia vifaa na vitendea kazi ambavyo vitawasadia katika shughuli zao za kiuchumi katika uzalishaji mali.

Mwenye ulemavu mwingine, Mshikila Juma, alisema licha ya kusoma bado wanakosa kazi katika taasisi mbalimbali kwa sababu ya ulemavu walionao na ili kuondokana na tatizo hilo wameamua kujiajiri wenyewe kupitia shughuli ndogo ndogo.

Naye mwakilishi wa wazee, Ramadhan Salehe alisema, kitendo cha mgodi huo kuwapatia bima za afya kinatakiwa kuigwa na wawekezaji wengine.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama Festo Kiswaga akikabidhi baiskeli na vifaa mbalimbali ambavyo vimetolewa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu kwa watu wenye Ulemavu kutoka vijiji vinavyozunguka Mgodi wa Bulyanhulu mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC : Wanafunzi endelezeni vita dhidi ya rushwa ngono

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewataka wanafunzi wanachama wa klabu za kupinga rushwa mkoani hapa kuendeleza jithada za mapambano ya rushwa ya ngono kwenye maeneo wanayotoka.

Shekimweri alitoa ushauri huo wakati wa mahafali ya wanafunzi wa kidato cha sita ambao ni wanachama wa klabu za kupinga rushwa yaliyofanyika katika Sekondari ya Dodoma.

Shekimweri alisema rushwa ya ngono bado ni kikwazo kikubwa kwa watoto wa kike hali inayokwamisha ndoto zao.

"Rushwa ya ngono bado ipo katika maeneo mbalimbali husani kwenye chaguzi na kwingineko ndio maana nasisitiza muende mkawe kioo cha jamii dhidi ya mapambano ya rushwa kwa sababu elimu ya uelewa ya athari za rushwa mnayo,"alisema Shekimweri.

Alisema uanachama wao usiishie hapo baada ya kuhitimu masomo yao,wanachotakiwa ni kwenda kuendeleza katika maeneo wanayotoka ili kusaidia wananchi kutambua namna rushwa inavyoleta madhara katika jamii.

Aliitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kushirikiana na jamii ili kuwa mabalozi wazuri wa kupinga vitendo vya rushwa.

Aliipongeza taasisi hiyo kwa kuanzisha klabu za wapingwa rushwa shuleni na vyuoni, na kuitaka kuongeza jitihada ili wanafunzi wengi wajiunge na klabu hizo.

Alisema kuwa idadi ya wanafunzi wanaohitimu kidato cha sita ni wengi lakini wanachama waliopo bado hawatoshi hivyo wanapaswa kuongeza jitihada ya kuongeza wanachama katika shule mbalimbali ambao watakuwa mabalozi wazuri wa mapambano dhidi ya rushwa hapo baadae.

Naye, Kamanda wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema taasisi hiyo imeelekeza nguvu zake katika mapambano dhidi ya rushwa ikiwamo kuwapa elimu jamii ya masuala ya kupiga vita rushwa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Kibwengo alisema moja ya mkakati ambao wamekuwa wakitumia katika kuelemisha jamii ni kampeni ya 'Ulipo Twaja' ambayo inawafikia wananchi popote walipo na kupewa elimu ya masuala ya kupiga vita rushwa ambayo inachangia kurudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi.

Kibwengo aliwataka wanafunzi kwenda kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwenye maeneo wanayotoka baada ya kuhitimu masomo yao.

Nipashe

# Spotika



KLABU 10 ZENYE MAPATO MAKUBWA ZAIDI ULAYA UK. 12



# NYOTA 6 WENYE ASISTI NYINGI 2022

**LONDON, England**

KATIKATI ya msimu ndipo wachezaji wengi huwa kwenye kiwango chao cha kupata mdundo mzuri. Baadhi ya wachezaji wa soka hupiga hatua zaidi uwanjani na wanaweza au wasiweze kuwa na matokeo madogo katika kipindi cha msimu. Lakini katikati ya msimu ndipo maandalizi ya mwisho wa biashara ya kampeni huanza.

Hapo ndipo unapohitaji wachezaji wako bora kuendeleza kiwango chao na wale ambao wamekuwa kimya hadi wakati huo waanze kufanya vizuri.

Sote tunajua ni wachezaji gani waliofanya vizuri zaidi msimu wa 2021-22 hadi sasa. Lakini ni wachezaji gani wamekuwa kwenye kiwango bora tofauti kabisa na mwanzo wa msimu?

Hapa tunawaangalia wachezaji sita waliotoa pasi nyingi zaidi za mabao (assists)kwa mwaka 2022 katika ligi tano bora za Ulaya (kwenye mashindano yote).

**#6. Mason Mount (Chelsea) - Asisti 7**

Chelsea walionekana kuwa hatarini katika nusu ya msimu. Lakini wameweza kupata kiwango bora cha Mason Mount na amekuwa muhimu kwa ushujaa wake tangu mwanzoni mwa mwaka.

Mount ndiye mtengenezaji mzuri wa mabao pale Chelsea na ameboresha kiwango chake cha uchezaji kwa kiasi kikubwa mwaka huu. Ametoa pasi saba za mabao katika mechi 17 kwenye mashindano yote mwaka huu.

**#5. Andy Robertson (Liverpool) - Asisti 7**

Beki wa kushoto wa Liverpool, Andy Robertson, bila shaka ni mmoja wa mabeki bora zaidi wa pembeni duniani kwa sasa na amedumisha kiwango chake kwa takriban miaka mitano sasa. Robertson ni mchezaji mkali kwa upande wa kushoto kwa kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp. Anapiga juu na chini bila kuchoka, lakini mchango wake ndio unaomtofautisha na wengine.

Katika mfumo wa mbinu wa Klopp, mabeki wa pembeni wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold na Andy Robertson, wanapewa mzigo wa kutengeneza nafasi. Wote wawili Robertson na Alexander-Arnold ni wapiga pasi wazuri wa mpira na wanaweza kupiga mipira ya kupendeza ndani ya kisanduku wapendavyo.

Robertson ametengeneza pasi saba za mabao katika mechi 16 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na Liverpool mwaka huu.

**#4. Christopher Nkunku (RB Leipzig) - Asisti 7**

Christopher Nkunku amejidhihirisha kuwa mmoja wa washambuliaji wa kufurahisha zaidi katika ligi tano kuu za Ulaya msimu huu. Amekuwa tishio kubwa mbele ya lango la wapinzani na nguzo muhimu ya mabao kwa RB Leipzig.

Nkunku ametoa pasi saba za mabao katika mechi 15 kwenye michuano yote mwaka huu. Miamba kadhaa ya Ulaya tayari iko kwenye foleni ili kumsajili msimu huu wa majira ya joto. Kwa mujibu wa ESPN, Liverpool, Manchester United, Arsenal na Paris Saint-Germain zote zimeonyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Katika mechi 40 kwenye michuano yote hadi sasa, Nkunku amefunga mabao 27 na kutoa asisti 17 msimu huu.

**#3. Benjamin Bourigeaud (Stade Rennais) - Asisti 7**

Kiungo wa kati wa Stade Rennais Benjamin Bourigeaud ni mchezaji ambaye jina lake halitajwi sana. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anaweza kucheza katika nafasi yoyote katika eneo la kiungo na ni mmoja wa wanasoka mahiri zaidi katika Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Bourigeaud ni mzuri akiwa na mpira miguuni mwake na pia anaweza kupiga mikwaju ya faulo. Mfaransa huyo amepanda kiwango chake mwaka 2022 na amekuwa katika kiwango cha hali ya juu katika wiki za hivi karibuni, huku akipiga hat-trick katika ushindi wa mabao 6-1 wa Rennes dhidi ya Metz Machi 20.

Ametoa asisti saba katika mechi 13 katika mashindano yote akiwa na RB Leipzig mwaka huu wa 2022.

**#2. Domenico Berardi (Sassuolo) - Asisti 7**

Domenico Berardi amekuwa mmoja wa mawinga bora katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa miaka sasa. Alikuwa kwenye kiwango bora wakati Italia ikishinda taji la euro 2020. Mshambulizi huyo wa Sassuolo yuko tayari kuhamia klabu kubwa zaidi mwishoni mwa msimu huu, huku AC Milan ikionyesha nia ya kutaka huduma yake, kwa mujibu wa gazeti la Calciomercato.

Berardi ni winga hatari ambaye anaweza kufanya yote katika nafasi tatu za mwisho. Anaweza kuwapita mabeki, kujiweka sawa kwa kupiga shuti au kucheza sehemu ya ulinzi.

Berardi ametoa asisti saba katika mechi 11 alizocheza kwenye mashindano yote mwaka huu wa 2022.

**#1. Ousmane Dembele (Barcelona) - Asisti 8**

Ousmane Dembele kwa sasa anatazamiwa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu. Barcelona na kambi ya mchezaji huyo hawakuweza kufikia makubaliano juu ya masharti ya mkataba mpya na mchezaji huyo.

Dembele amekuwa mchezaji bora wa Barcelona mwaka 2022. Amecheza soka bora zaidi maishani mwake chini ya kocha Xavi Hernandez katika miezi ya hivi karibuni.

Dembele ametoa pasi nane za mabao katika mechi 14 alizocheza hadi sasa mwaka huu. Kutokana na hali hiyo, Barcelona sasa wanatarajiwa kuanzisha upya mazungumzo ya mkataba mpya na Dembele kwa nia ya kumfunga katika klabu hiyo kwa muda mrefu.

## ISIKUPITE

01/08 - Siku hii mnamo 1970, David James alizaliwa. Ndiye golikipa aliyecheza mechi nyingi zaidi (572) za Ligi Kuu England (Premier League), kuliko kipa mwingine yeyote katika historia ya ligi hiyo.



NIPASHE JUMATATU APRILI 11, 2022



## Extra Time




Manchester City

# KLABU 10 ZENYE MAPATO MAKUBWA ZAIDI ULAYA

**LONDON, England**

KAMPUNI ya Deloitte Football Money, huorodhesha klabu za soka kulingana na mapato yanayotokana na shughuli zao zinazohusiana na mpira wa miguu.

Sasa wametoa orodha ya klabu tajiri zaidi Ulaya kwa msimu wa 2020-21 na kuna mambo kadhaa ya kushangaza.

Kwa mujibu wa Deloitte janga la COVID-19 bila shaka limekuwa na athari kubwa kwa mapato ya fedha kwa klabu.

"Ingawa kwa kawaida tungehusisha COVID-19 na athari mbaya ya kifedha, si vyanzo vyote vya mapato vilipungua ikilinganishwa na msimu uliopita, na mapato ya jumla ya rekodi (euro bilioni 4.6) yamerekodiwa.

"Mtazamo si mzuri kama unavyoweza kuonekana, pamoja na kuongezeka kwa mapato ya matangazo katika msimu wa 2020/21 kutokana na athari za pande mbili za kuahirishwa kwa utangazaji, kumekuwa na ongezeko la haki ya matangazo," imenukuliwa taarifa ya Deloitte.

Sasa hapa tunaangalia klabu 10-bora zilizo na mapato ya juu zaidi.

**#10. Tottenham Hotspur**

Tottenham Hotspur imeshuka kutoka nafasi ya nane hadi ya kumi katika orodha ya mwaka huu. Kumekuwa na mabadiliko ya asilimia tisa katika jumla ya mapato yao ya kila mwaka.

Jumla ya mapato yaliyopatikana kwa Spurs ni euro milioni 406.2, huku kukiwa na salio lao la uhamisho la hasi euro milioni 103.1.

**#9. Juventus**

Juventus wamepanda kutoka nafasi ya 10 hadi ya tisa katika viwango vya ubora wakati huu. Wamepata jumla ya mapato ya kila mwaka ya euro milioni 433.5, ambayo kumekuwa na ongezeko la asilimia tisa kutoka mwaka jana. Uwiano wao wa mshahara kwa mapato ni asilimia 74 na salio lao la uhamisho ni hasi euro milioni 93.3.

**#8. Chelsea**

Chelsea ilimaliza msimu wa 2020-21 kwa njia nzuri kwa kuwa mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Yalikuwa mafanikio makubwa sana kwa Kocha Thomas Tuchel, ambaye aligeuza msimu wa 'Blues' hao baada ya kuteuliwa mwishoni mwa Januari 2021.

Jumla ya mapato ya Chelsea kwa mwaka ni euro milioni 493.1, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia tano kutoka mwaka jana. Uwiano wa mshahara kwa mapato ni asilimia 77. Chelsea walitumia muda mwingi kwenye dirisha la usajili, na salio lao la uhamisho ni kubwa ambalo ni hasi euro milioni 214.

**#7. Liverpool**

Liverpool wameshuka nafasi mbili na kushika nafasi ya saba mwaka huu. Wameshuka kwa asilimia moja ya mapato yao. Jumla ya mapato yao ya kila mwaka yalikuwa ni euro milioni 558.6 kwa mwaka jana, lakini yameshuka hadi euro milioni 550.4 wakati huu. Uwiano wao wa mshahara kwa mapato ni asilimia 64.

**#6. Paris Saint-Germain**

Paris Saint-Germain wamefanikiwa kupanda kutoka nafasi ya saba hadi ya sita mwaka huu. Jumla ya mapato yao ya kila mwaka ni euro milioni 556.2 maana yake yamepanda kwa asilimia tatu kutoka mwaka jana. Uwiano wa mshahara kwa mapato ya PSG haupatikani, lakini kuna uwezekano ukawa juu sana kwani wana wachezaji wakubwa kama Lionel Messi, Neymar, Kylian Mbappe na Marco Verratti.

**#5. Manchester United**

Manchester United ni moja ya klabu maarufu duniani. Jumla ya mapato yao ya kila mwaka yameshuka kwa asilimia nne, ikishuka kutoka euro milioni 580.4 mwaka jana hadi euro milioni 558 mwaka huu. Uwiano wao wa mshahara kwa mapato unasimama kwa asilimia 65.

Wakiwa wametumia gharama kubwa katika dirisha la usajili la majira ya joto, salio lao la jumla la uhamisho ni hasi euro milioni 106.2.

**#4. Barcelona**

Matatizo ya kifedha ya Barcelona yamerekodiwa vema katika miaka michache iliyopita. Timu hiyo kutoka Katalunya iliongoza orodha ya mapato makubwa mara ya mwisho, lakini wameanguka nafasi tatu na wako kwenye nafasi ya nne wakati huu. Jumla ya mapato yao ya kila mwaka yalisimama kwa euro milioni 715.1 mwaka jana. Yameshuka hadi euro milioni 582.1 wakati huu na ni sawa na kushuka kwa asilimia 18.

Uwiano wa mshahara kwa mapato wa Barcelona pia ni wa juu sana kwa asilimia 84. Salio lao la jumla la uhamisho ni hasi euro milioni 24.

**#3. Bayern Munich**

Bayern Munich imekuwa moja ya timu zilizofanikiwa na kutawala zaidi barani Ulaya katika miaka michache iliyopita. Wamekaa kwenye nafasi ya tatu katika orodha ya mwaka huu. Wameshuka kwa asilimia nne kwa jumla ya mapato yao ya kila mwaka. Yameshuka kutoka euro milioni 634.1 hadi euro milioni 611.4.

Bayern Munich kwa sasa wako mbioni kushinda taji lingine la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na wamefanikiwa kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#2. Real Madrid**

Real Madrid pia wamefanikiwa kushika nafasi ya pili kwenye orodha ya mwaka huu. Lakini mapato yao ya jumla ya kila mwaka yameshuka kwa asilimia saba kutoka euro milioni 714.9 mwaka jana hadi euro milioni 640.7 wakati huu.

Uwiano wao wa mshahara kwa mapato ni asilimia 63. 'Los Blancos' hao wamekuwa waangalifu kuhusu kutumia fedha kwenye madirisha ya usajili na wana salio la kuvutia la uhamisho la chanya euro milioni 86.8.

**#1. Manchester City**

Manchester City wameingia kileleni mwa orodha hiyo kwa mara ya kwanza katika historia. Jumla ya mapato yao ya kila mwaka yalisimama kuwa euro milioni 549.2 kwa mwaka jana. Yamepanda kwa asilimia 17 na kuwa euro milioni 644.9 wakati huu.


Uwiano wao wa mshahara kwa mapato ni asilimia 62. Lakini salio lao la jumla la uhamisho ni hasi euro milioni 112.4. Manchester City wameshinda taji la Ligi Kuu England katika misimu mitatu kati ya minne iliyopita na ni moja ya timu zenye nguvu barani Ulaya hivi sasa.

## Nukuu

Kutokana na hatihati ya kumkosa Bernard Morrison (mechi ya marudiano Sauzi), tunahitaji kumaliza mechi yote Uwanja wa Benjamin Mkapa Aprili 17 (Jumapili wiki hii), tunataka kukamilisha kila kitu nyumbani, tunataka kwenda ugenini tukiwa na uhakika mkubwa wa ushindi wa nyumbani," **Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez**



"Jana, ilinipitia akilini kwamba naweza kucheza tena. Inter Miami walinipigia simu lakini nilikataa. Katika miaka miwili? Ngoja tuone. Madaktari waliniambia kuwa ninapaswa kutumia miezi mitano au sita bila shughuli, lakini tayari ninataka kufanya mazoezi. tena!," **Mshambuliaji wa zamani wa Barcelona na Manchester City, Sergio Aguero akidokeza uwezekano wa kurejea kwenye soka.**



"Sina hakika jinsi Brazil na Argentina zilivyo na nguvu kwa wakati huu, lakini Ulaya, Italia hawapo. Hispania, sidhani kama wanatosha kushinda pia. Ujerumani, huwezi kujua wanaweza kushinda. Ubelgiji ni timu nzuri kila wakati. Kundi la England, Iran, Marekani na kisha ni Ukraine Scotland au Wales. Ninamaanisha, siku zote ni vigumu katika Kombe la Dunia, lakini siwezi kuwaona (England) hawashindi kundi hilo," **Kocha wa zamani wa England, Sven-Goran Eriksson na mtazamo wake kuhusu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar.**



## MAHOJIANO MAALUM

# CHAMBUA: UBORA NA UDHAIFU WA SIMBA UPO HAPA

- Atoa angalizo kwa Yanga ubingwa Ligi ya NBC
- Aweka msimamo nafasi ya uchawi katika soka

**Na Sanula Athanas, DODOMA**



Sekilojo Chambua (kushoto), na nyota wa zamani wa Taifa Stars, Adolf Rishard, wakiwa wameshika Kombe la Dunia wakati lilipotembezwa hapa nchini kabla ya kuanza fainali za michuano hiyo nchini Afrika Kusini mwaka 2010. **PICHA: MAKTABA**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Yanga, Sekilojo Chambua, amezungumza na Nipashe kuhusu maisha yake ya kisoka, akiwa na angalizo kwa wachezaji vijana nchini kwamba ajira ya soka ni ya kipindi kifupi.

Katika mahojiano maalumu na Nipashe iliyomnasa hivi karibuni jijini Dodoma akiendelea na majukumu yake mapya, Chambua aliyewahi kuwa Kocha Msaidizi wa Yanga chini ya Kocha Mkuu, Mmalawi Jack Chamangwana, alitoa mbinu kwa Simba kuimaliza Orlando Pirates katika mechi inayofuata ya hatua ya robo-fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

*Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mshambuliaji huyo wa zamani wa Tukuyu Stars na Taifa Stars ambaye Yanga walimtumia pia katika nafasi ya winga wa kulia:

**SWALI:** Unaiona Simba ikifika wapi katika michuano ya CAF msimu huu na je, mbio zake za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu zipo au zimeisha?

**CHAMBUA:** Kwenye mpira wanasema chochote kinaweza kutokea. Kwa hiyo, kwenye michuano hii ya CAF ambayo Simba wanacheza, ukiangalia bado wana nafasi ya kufanya vizuri.

Kinachotakiwa kwa wachezaji na uongozi mzima wa Simba, ni 'seriousness' (umakini) uongezeke, nafasi watakazopata wazitumie ipasavyo na wapate magoli mengi nyumbani maana mechi za Afrika inaonekana kila mtu anashinda nyumbani kwake.

Kwa hiyo, Simba wanayo nafasi ya kufanya vizuri katika michuano ya Afrika msimu huu. Kwa Ligi Kuu ya Tanzania Bara, Yanga ina nafasi kubwa kutwaa ubingwa, lakini isitetereke.

Simba wanashika nafasi ya pili na katika mpira wa miguu, bado wanayo nafasi ya kutetea ubingwa iwapo Yanga itatetereka na wao Simba wafanye vizuri katika mechi zilizobaki.

Yote kwa yote, ninaweza kusema kwamba Simba wanayo nafasi kwa kuzingatia mazingira ya kimpira, unaweza kusema bado wana nafasi hiyo katika ligi ya nyumbani.

**UBORA, UDHAIFU WA SIMBA**

Ninapoitazama mechi inayofuata ya Simba CAF, ninaona itategemea na namna wanavyojipanga kucheza mechi yenyewe. Kama mchezaji wa zamani, ninaona chochote kitatokea.

Kama watajipanga vizuri hasa kwa mechi ya nyumbani, wanatakiwa wahakikishe wanapata magoli mengi, wapate magoli zaidi ya mawili, hapo watakuwa na nafasi nzuri ya kushinda.

Simba wana nafasi, lakini Orlando pia wana nafasi. Ninaamini atakayetumia vizuri mechi ya kwanza ndiye atafuzu kwenda hatua ya nusu fainali.

Ubora wa Simba kwa sasa uko kwa mlinda mlango, wana kipa mzuri. Safu yao ya ulinzi ni nzuri, lakini imesheheni wachezaji wenye umri mkubwa, ni kweli wana uzoefu mkubwa, lakini umri umewatupa.

Ukitazama umri wa Shomari Kapombe ni mkubwa, kuna Pascal Wawa na Onyango, kuna Erasto Nyoni, hiyo ni safu ya ulinzi ambayo Simba wanaitumia kwenye mechi mbalimbali. Wana uzoefu lakini umri umewatupa. Wakikutana na timu yenye kasi wanapata shida!

Safu yao ya kiungo ina watu wazuri, yupo Morrison ambaye kule Afrika Kusini hawezi kucheza kutokana na matatizo yake na wale watu wa Afrika Kusini.

Washambuliaji wao kama Kagere ni wazuri, wana ari ya upambanaji, lakini umri unawatupa. Yupo Mugalu, ni kijana ambaye ninaamini ataendeleza makali aliyoyaonyesha katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi.

Kwa hiyo, Simba ina ubora na udhaifu katika maeneo hayo niliyokutajia, Orlando Pirates siwajui kwa kina sana, lakini nimeangalia mechi zao kadhaa. Simba ichunge sana mashambulizi ya kushtukiza. Wana tabia ya kuvuta, lakini wakushambulia ghafla na kwa kasi, Simba wawe macho sana kuwakabili vijana wao wenye kasi.

**SWALI:** Kumekuwa na dhana kwamba katika soka kuna uchawi. Kwa mtazamo wako unadhani uchawi una nafasi kwenye soka? Ulipokeaje na ulikuwa unajisikiaje pale vitu kama hivyo vinapotendeka?

**CHAMBUA:** Unajua hili ni suala la imani. Wapo watu ambao wanasema uchawi upo, lakini kwa upande wangu sikuwahi kulithibitisha hilo na maisha yangu ya soka yalikuwa ya kumtegemea zaidi Mungu muda wote kuanzia nilipokuwa Tukuyu Stars ya Mbeya na Yanga, hata nilipokuwa kwenye timu ya taifa.

Kiujumla ni kwamba, maisha yangu yalikuwa ya kumtegemea zaidi Mungu, kusali wakati wa mazoezi, kusali wakati wa kwenda kucheza mechi mbalimbali. Hivyo ndivyo ambavyo nimekuwa nikiamini na sikuwahi kuthibitisha mambo hayo kwa sababu siyapi nafasi.

Ninaamini zaidi katika kujituma katika mazoezi na wakati wa mechi pamoja na kuwa mbunifu zaidi muda wote unapokuwa uwanjani.

**SWALI:** Ukiwa Yanga ulipita chini ya makocha mbalimbali wakiwamo Tambwe Leya, Tauzany Sunday Kayuni na Mwaluvanda. Unawazungumziaje makocha hawa?

**CHAMBUA:** Nimepita katika makocha wengi walionifundisha katika Klabu ya Yanga. Siyo hao tu uliowataja, wako makocha wengi wakiwamo wazungu, kulikuwa na Mmalawi Chamangwana, huyu nilifanya naye kazi akinifundisha akiwa mwalimu na badaye nilipostaafu kucheza nikawa msaidizi wake niliposomea ukocha.

Kila kocha ana falsafa yake, nimefaidika sana na falsafa hizo za kila mwalimu katika kipindi changu cha soka tangu nilipojiunga na Klabu ya Yanga hadi nilipostaafu mwaka 2003.

Kwa kifupi, niseme tu kila mwalimu alikuwa na falsafa yake na mchango mkubwa kwa maendeleo yangu hadi hapa nilipofika.

**SWALI:** Zidane, Thiery Henry na hata Beckham wamestaafu soka katika umri unaoonekana mdogo. Ni upi ushauri wako kwa wachezaji wa soka nchini?

**CHAMBUA:** Ushauri wangu kwa vijana ni kujipanga mapema maana mpira ni ajira ya kipindi kifupi. Hili ni jambo ambalo vijana wengi wa Kitanzania hawalijui. Kwa hiyo, rai yangu kwao ni hii, kwamba ni vizuri wakajipanga mapema ili waache mpira mapema wakati bado wanaweza.

Lipo tatizo kubwa nchini kwamba unatengeneza jina kubwa, lakini baadaye unang'ang'ania kuendelea kucheza kwa sababu huna kipato bado hakijatimia ilhali mwili unakuzuia kuendelea na mpira.

Kuna matatizo mengi yanayosababisha watu waendelee kung'ang'ania kucheza, ikiwamo hali ya vipato vya timu zetu, ukiondoa hizo klabu kubwa.

Kwa hiyo, unakuta mchezaji alikuwa na jina kubwa, lakini anaendelea kung'ang'ania kucheza mpira hata katika umri mkubwa, mwishowe anapata aibu ya kuzomewa na mashabiki 'toa huyo, toa huyo'.

Kusema kweli hiki siyo kitendo kizuri. Kwa hiyo, wajipange waache mpira katika kipindi ambacho mashabiki bado wanawahitaji. Huu ndiyo utaratibu mzuri ambao wenzetu wa Ulaya na Amerika wanaufanya.

**SWALI:** Umri wako kimwonekano ni tofauti na unaoonekana kwenye hati yako ya kusafiria ukiwa na Taifa Stars, kwa maana sasa kwa mujibu wa hati hiyo, una miaka 44 tu. Shida ni nini?

**CHAMBUA:** ... (kicheko). Hakuna shida yoyote lakini kwa wachezaji wa Kiafrika kwa kipindi kile na hata sasa wanaotaka kucheza Ulaya, wakati mwingine wanapunguza umri kwa ajili ya soko la Ulaya.

Kwa hiyo, siyo kitu kibaya. Kimwonekano kwangu kunatokana na kujitunza, ni kitu muhimu sana kwa mchezaji kwa sababu muda mwingi anakuwa mfanyaji wa mazoezi, lakini lazima pia kujitunza vizuri kwa maana ya kuwa na nidhamu katika maisha.

Hapa nina maana mchezaji lazima ujipende, inakusaidia kukufanya uonekana bado kijana na mtu mwenye nguvu kuliko wale ambao baada ya kuacha mpira, hawajitunzi. Kujitunza maana yake ni kuepuka ulevi, zinaa, kutokula vizuri na mambo yanayofanana na hayo.

***ITAENDELEA JUMATATU IJAYO**

**JE, WAJUA?**



MAKIPA wanaoongoza kwa michezo mingi bila kuruhusu bao (clean sheets) kwenye Ligi Kuu Tanzania kwa msimu huu wa 2021/2022 ni Kipa wa Yanga, Djigui Diarra mwenye clean sheets 10, Aishi Manula wa Simba (9), Aboutwaleeb Mshery wa Yanga (8) na golikipa wa Biashara United, Cleo James Ssetuba (7).





# Mpango waongeza ufaulu shule za msingi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTAFITI umebaini Mpango wa Uboreshaji Elimu Kupitia Mafunzo ya Ualimu Kazini (SITT) uliotekelezwa kwa shule mbalimbali za msingi nchini umechangia ongezeko la ufaulu wa alama za juu kwa asilimia 30, huku kufeli kukipungua kwa asilimia 10.

Mhadhiri na Mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Bern, Idara ya Uchumi na Utafiti nchini Uswisi, Dk.Konstantin Büchel alitoa kauli hiyo alipokuwa akiwasilisha matokeo ya tathmini ya mradi huo unaofadhiliwa na Chama cha Walimu Tanzania(CWT) kwa kushirikiana na Shirika la Helvetas.

Alisema idara hiyo hufanya utafiti wa masuala ya maendeleo na elimu kwenye nchi mbalimbali ambapo kupitia Shirika la Helvetas lilifanya tathmini ya mradi wa SITT.

"Tuliamua kufanya utafiti ili kuona matokeo ya mradi huu katika shule mbalimbali, tulishirikiana na Helvetas Tanzania katika kufanya tathmini kwenye wilaya za Mbulu, Karatu, Mbulu Mji na Siha ambapo tulishirikisha walimu, wanafunzi, viongozi ambao wameonyesha kufurahia mradi na wapo tayari kubeba na kuendeleza zaidi kwa ajili ya manufaa ya wanafunzi na walimu," alisema.

Alisema katika tathmini waliyofanya wamegundua mradi unaleta tija katika ufundishaji na ujifunzaji kutokana na walimu kushirikiana, kuwa huru kufundisha na wanawapa wanafunzi nafasi kubwa kama chanzo cha maarifa.

"Tumeona ushirikishaji huo wa wanafunzi shule za mradi zimefanya vizuri katika matokeo ya mtihani wa darasa la saba na la nne, na tumegundua ongezeko la alama za juu yaani 'A' na 'B' zimeongezeka katika shule za mradi kwa asilimia 30 na kufeli kumepungua kwa asilimia 10, hivyo mradi unaonesha kuleta tija ikilinganishwa na maeneo mengine,"alisema.

Naye, Meneja Mradi huo, Donatian Marusu, alisema mradi huo umefikia shule 408 na walimu 892 kwenye mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Tabora, Singida, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Mkuu wa Idara ya Elimu na Mafunzo CWT, Stella Kiyabo, alisema mradi huo unafundisha walimu mbinu rahisi za kufundishia masomo ya Hisabati, Kiingereza, Sayansi na unajihusisha na masuala ya afya na mazingira.

"Tumetaka wafanye kazi zao kwa urahisi bila kuogopa mada yeyote kwa madai kuwa ni ngumu, CWT inaionesha serikali umuhimu kuwa na mafunzo kazini kwa walimu,"alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Helvetas nchini, Annet Witteveen, alisema kuna haja ya kupeleka mradi huo kwenye mikoa mingine ya Lindi, Geita, Mtwara na Morogoro ili kuhakikisha wananchi wanapata mbinu mbalimbali za ufundishaji.

Mmoja wa walimu walionufaika na mafunzo hayo, Mwalimu Diana Zakaria kutoka Shule ya Msingi Ololieni Mkoa wa Arusha, alisema mradi huo umewajengea uwezo wa kufundisha wanafunzi wengi wanaokuwa kwenye chumba kimoja kwa kuwaweka kwenye makundi mbalimbali na kufundisha zaidi ya mada moja.

"Mradi wa SITT unamfanya mwalimu kujishusha kuwa sawa na wanafunzi ili kutambua matatizo mbalimbali ya wanafunzi na kuzitatua hii imesaidia kuongeza ufaulu,"alisema.



Mkurugenzi Mkazi wa Kampuni ya kimataifa ya kusafirisha mizigo ya DHL, Paulo Makolosi (kushoto) akimkabidhi Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdalla Ulega boti ya doria ya uvuvi kwenye hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki mkoani Kigoma. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dk. Rashid Tamatamah. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kazi za viongozi kuendelea kuhifadhiwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuhifadhi kazi mbalimbali za viongozi wa nchi kwa lengo la kurithisha vizazi vijavyo na kivutio cha utalii.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Juma Mkomi alitoa ahadi hiyo juzi alipopokea msafara wa waendesha baiskeli wa twende Butiama ulipopita ofisi ya Wizara hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 100 ya maisha ya Mwalimu Julius Nyerere.

"Kazi ya serikali kupitia wizara yetu ni kuhifadhi kumbukumbu na kazi za viongozi wote zinahifadhiwa ili kuwa sehemu ya kivutio cha utalii nchini,"alisema.

Alibainisha kuwa serikali inafanya maadhimisho ya miaka 100 ya maisha ya rais huyo wa kwanza wa Tanzania kwa sababu kazi zake alizofanya wakati wa uhai wake bado zinaendelea kuishi katika jamii.

Alizitaja baadhi ya kazi alizofanya Nyerere kuwa aliongoza harakati za ukombozi kwa nchi mbalimbali hadi zikajipatia uhuru na hakukubali wanyonge kuonewa. Naye kiongozi wa timu ya waendesha baiskeli ya Twende Butiama, Gabriel Landa, alisema timu yao ilianza safari Aprili 7,mwaka huu nyumbani kwa Mwalimu Nyerere eneo la Msasani mkoani Dar es Salaam na wanatarajia kutumia siku tano mpaka kufika Butiama mkoani Mara. Landa alisema safari yao inahusisha makundi mawili ambayo ni Julius Kambarage Festival linalowahusisha wasanii wa maigizo kutoka maeneo mbalimbali.

Aidha alisema lengo la safari yao ni kuhamasisha utalii wa ndani ambapo wamekuwa na utaratibu wa kutangaza vivutio hivyo katika safari zao na walishafanya safari ya Mikumi ,

Ngorongoro na Kolo. Kwa upande wake, Mkurungenzi wa Mali Kale wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Kristowaja Ntandu alisema katika maadhimishi hayo kuna makundi mbalimbali ya vijana wanaendelea na matembezi kutoka Mwanza kuelekea Butiama.

Ntandu alisema katika kuadhimisha miaka 100 ya maisha ya Mwalimu Nyerere wizara iliunda kamati ya Kitaifa ambayo ilifanya kazi ya kutangaza kazi alizowahi kuzifanya wakati wa uhai wake.

Kadhalika, alisema hitimisho la kilele cha maadhimisho hayo kitakuwa Aprili 13, mwaka huu nyumbani kwake Butiama.

# Bil. 236/- za kesi zaokolewa mwaka mmoja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Wakili Mkuu wa Serikali imeokoa Sh. bilioni 236.6 ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kushinda mashauri 450 ya madai na usuluhishi.

Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, aliyasema hayo jana kwenye Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo lililofanyika jijini hapa.

Alisema Ofisi hiyo imeendesha mashauri 1,219 ambapo kati ya hayo ya madai ni 1,102 na ya Usuluhishi 117.

"Aidha, Mashauri ya Madai yaliyomalizika hadi Januari 2022 na Serikali kushinda ni 444 na Mashauri ya Usuluhishi 6 na hivyo kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 236.6,"alisema.

Kadhalika, alisema kwa kipindi hicho Ofisi hiyo imeimarisha mfumo wa kukusanya takwimu za kesi, kufanya ufuatiliaji wa mienendo ya kesi na kupitia sheria zinazohusu kesi za madai na usuluhishi.

"Pia Ofisi imeweza kuandaa miongozo ya kusimamia na kuthibiti viwango vya ubora vya Mawakili katika uendeshaji wa kesi.Vile vile, Ofisi imeweza kuandaa mkataba wa Huduma kwa Mteja ambao ni Serikali na taasisi zake,"alisema.

Akizungumzia kuhusu kero zinazoikabili ofisi hiyo, Malata alisema inakabiliwa na upungufu wa watumishi 153 kwa mujibu wa ikama iliyopo kwa sasa ambayo ina Watumishi 312.

" Maslahi kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili wa Serikali hayaendani na uzito wa majukumu ya ofisi, ufinyu wa bajeti, kukosekana kwa mawakili wenye stadi maalumu kwenye maeneo mtambuka,"alisema.

Hata hivyo alitaja mikakati mbalimbali ya ofisi hiyo ikiwamo kuendelea kuwajengea uwezo Mawakili katika kuandaa utetezi na kuhakikisha kuwa wanawatumia Mawakili wa ndani kuendesha kesi zote za ndani na nje ya nchi pale ambapo sheria zinaruhusu kufanya hivyo.

Akifungua kikao hicho, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geofrey Pinda, alitaka bajeti itakayotengwa kwa ajili ya taasisi hiyo kuzingatia malengo na rasilimali zinazokadiriwa kutumika.





## DC aagiza ulinzi chanzo cha maji Mto Nzovwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, ameagiza viongozi wa Kata ya Mwakibete katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya kushirikiana na wananchi kupanda miti kwenye chanzo cha maji cha Mto Nzovwe II ili kukilinda.

Dk. Chuachua alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazindua kampeni ya upandaji wa miti katika Kata hiyo ambapo aliwataka kwenda kuchukua miti iliyooteshwa katika Ofisi za Wakala wa Usimamizi wa Misitu nchini (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema chanzo cha maji cha Mto Nzovwe ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya maji vinavyosaidia wananchi wa Jiji la Mbeya kupata huduma ya maji ya kutosha.

Alisema maeneo yote yanayozunguka chanzo hicho yanatakiwa kupandwa miti ambayo ni rafiki kwenye vyanzo vya maji huku akiwataka maofisa wa TFS kuwaongoza wananchi hao.

"Mwanzo niliagiza kwamba wananchi wakachukuwe miti kwenye ofisi za TFS, lakini sasa nimebadili utaratibu, TFS watawaletea miti hapa ili mshirikiane kupanda chini ya maelekezo yao," alisema Dk. Chuachua.

Alisema maeneo mengi ya chanzo hicho yako wazi hali ambayo inasababisha baadhi ya wananchi kuyafanya kuwa maeneo ya kuchungia mifugo hali inayochangia uchafuzi wa maji yanayotumiwa na wananchi.

Diwani wa Kata ya Mwakibete, Lucas Mwampiki, aliahidi kushirikiana na wananchi wake pamoja na maofisa wa TFS kupanda miti hiyo kwa maelezo kuwa wao ni miongoni mwa wanufaika wa chanzo hicho na hivyo wana wajibu wa kukilinda.

Alisema mara nyingi wananchi wamekuwa wakiharibu vyanzo vya maji kwa sababu ya kukosa elimu sahihi ya vyanzo vya maji na hivyo akawaomba maofisa wa TFS na taasisi zingine zinazosimamia mazingira kutoa elimu kwa wananchi.

Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Cosmas Ndakidemi, alisema taasisi yake imeandaa miche ya kutosha na inagawa bure kwa wananchi wanaotaka kupanda kwa ajili ya kulinda mazingira.

Aliwataka wananchi wa Kata ya Mwakibete pamoja na maeneo mengine yanayozunguka vyanzo vya maji kwenda kuchukua miti hiyo na kuipanda kwenye vyanzo hivyo.

# Kilimo cha pilipili Mbarali kilivyowezeshwa

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

WAKULIMA wa pilipili kichaa katika Kijiji cha Ihahi kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wamepewa msaada wa kaushio la kisasa la pilipili zao linalotumia nishati ya jua ili kupunguza upotevu wa mazao yao.

Wakulima hao wamepatiwa kaushio hilo la kisasa na Shirika ka HELVETAS kupitia mradi wake wa kuwawezesha wanawake na vijana kwenye kilimo cha bustani na utafutaji wa masoko (KIBOWAVI) ya mazao wanayozalisha.

Msaada huo ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya Bustani ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) na Serikali ya Tanzania ambapo HELVETAS ni miongoni mwa watekelezaji.

Kwenye programu hiyo ya AGRI-CONNECT, EU inachangia asilimia 90 na Serikali ya Tanzania inachangia asilimia 10 ambapo pia inashughulika na uboreshaji wa miundombinu ya barabara za vijijini pamoja na kuboresha lishe kwa jamii.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kaushio hilo, mwakilishi wa kikundi cha wakulima hao, Tunsume Mwandupe, alisema awali walikuwa wanashindwa kukausha vizuri pilipili zao na hivyo kusababisha upotevu wa mazao yao. Alisema baada ya kupewa msaada wa kaushio hilo, wana uwezo wa kukausha mazao yao ndani ya muda mfupi na kuyauza hali ambayo imewasaidia kupunguza upotevu na kujiongezea kipato.

"Mpaka sasa tumeshaingia mkataba na mnunuzi wa pilipili kichaa zetu ambaye anakuja kuzinunua hapahapa baada ya kuzikausha, tunawashukuru sana KIBOWAVI, mbali na kutusaidia kaushio hili pia wametupatia mafunzo mbalimbali," alisema Tunsume.

Akizindua Kaushio hilo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbarali, Michael Semindu, alilipongeza Shirika la HELVETAS kwa kuwasaidia wakulima wa wilaya hiyo akisema wakulima wa maeneo hayo wana mwamko wa kulima lakini wamekuwa wakikosa nyenzo za kisasa za kuendeshea kilimo.

Alisema ofisi yake itahakikisha kikundi cha wakulima hao wa pilipili kinasajiliwa na kinakuwa miongoni mwa vikundi vinavyopewa kipaombele kwenye mikopo inayotolewa na Halmashauri pamoja na fursa zingine.

Alisema mbali na kuwasaidia wakulima hao kaushio lakini pia Shirika hilo la HELVETAS limesaidia kujenga ghala la kuhifadhia vitunguu vya wakulima wa Skimu ya Umwagiliaji ya Igomelo ambalo pia ni la kisasa. "Nashukuru kwamba maofisa wa Wizara ya Kilimo wapo hapa na wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), mmejionea wenyewe barabara zetu tunaomba mtusaidie ziboreshwe ili wakulima wasafirishe mazao yao vizuri kwenda sokoni," alisema Semindu.

Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo, Daines Mtei, alisema lengo la Serikali ni kuhakikisha wakulima wananufaika na mazao wanayozalisha na hivyo akaahidi Serikali kuendelea kuwatafutia wakulima fursa mahali popote ili wanufaike.

Alisema kabla ya kwenda kuzindua kaushio hilo walianzia kukagua barabara mbalimbali zinazohudumiwa na TARURA ili kuhakikisha zinaboreshwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa HELVETAS, Daniel Kalimbya, alisema shirika hilo pia limesaidia vikundi vingine makaushio hayo ya kisasa katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Songwe na Katavi.

Alisema lengo la mradi ni kuongeza uzalishaji, kuwaongezea wakulima kipato na kuboresha lishe ili kupunguza matatizo ya utapiamulo na udumavu wa watoto kwenye maeneo ya mradi.



Mwakilishi wa Wizara ya Kilimo, Daines Mtei (Katikati) pamoja na maofisa wa Shirika la HELVETAS na wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wakipokea maelezo kutoka kwa wakulima wa pilipili kichaa wa Kijiji cha Ihahi kuhusu matumizi ya kaushio la kisasa la pilipili ambalo wamepatiwa na Shirika la HELVETAS kupitia mradi wa KIBOWAVI. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Waiomba serikali kuipanua barabara ya TANZAM

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

WATUMIAJI wa mpaka wa Tanzania na Zambia katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe, wameiomba Serikali kupanua barabara kuu inayounganisha nchi hizo (TANZAM) kuwa ya njia nne ili kupunguza msongamano wa malori na kurahisisha upitishaji wa mizigo.

Wadau hao wameiomba serikali angalau iipanuwe barabara hiyo umbali wa kilomita 20 kutoka ulipo mpaka huo wakidai kuwa eneo hilo ndilo linakuwa na msongamano mkubwa, kutokana na malori mengi kuegeshwa wakati yanasubiri kukamilika kwa nyaraka za kuvuka.

Walitoa ombi hilo juzi wakati kikosi kazi cha wataalamu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kutoka makao makuu Dar es Salaam kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kilipotembelea mpaka huo kwa lengo la kukutana na wadau.

Kikosi kazi hicho kilikuwa na lengo la kukutana na wadau ili kujadiliana namna ya kuboresha huduma za bandari na kurahisisha biashara ya kimataifa kati ya Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Mwenyekiti wa madereva wa magari yanayosafirishwa (IT), Khalid Salim, alisema kwa sasa wateja wengi wa kutoka nchi za ukanda wa SADC wanapenda kupitishia mizigo yao katika Bandari ya Dar es Salaam, kutokana na kuwa na uhakika wa usalama wa mizigo yao.

Alisema kutokana na hali hiyo mizigo mingi imekuwa ikipitishwa katika bandari hiyo, hivyo kusababisha msongamano katika mpaka wa Tunduma, na akaomba barabara iboreshwe ili kuondoa tatizo la msongamano. Alisema endapo barabara hiyo itaboreshwa kutakuwa na ongezeko la biashara zaidi na Serikali itaongeza mapato katika mpaka huo, akisema muda ambao unatumika kusubiri ni sehemu ya upotevu wa mapato.

"Tunawaombeni sana bandari yetu imekuwa na mvuto kwa mataifa mengi, sasa tunaomba hii barabara iboreshwe ili kuondoa huu msongamano wa magari kwenye mpaka wetu, huu mji wa Tunduma kwa sasa una magari mengi sana," alisema Salim.

Mwakilishi wa Kampuni ya Usafirishaji ya Lead Trans, Jumanne Wabara, aliwashukuru maofisa wa kikosi kazi hicho kwa kuamua kufanya kikao cha pamoja na wadau katika mpaka huo na kusema kuwa na wao kiliwasaidia kuwasilisha kero zao.

Alisema kikao hicho kitaisaidia Serikali kujua mahitaji ya wadau wanaotumia mpaka huo pamoja na Bandari ya Dar es Salaam na bandari zingine.

Alisema pamoja na kwamba Serikali ina mpango wa kuipanua barabara ya TANZAM kutoka Igawa wilayani Mbarali mpaka Tunduma yenye urefu wa zaidi ya Kilomita 200, lakini ingeanzia katika Mji wa Tunduma kwa kujenga kipande kidogo.

"Zaidi ya asilimia 70 ya mizigo inayoshushwa katika bandari yetu ya Dar es Salaam inapita kwenye mpaka huu kwenda mataifa ya kusini, sasa msongamano unapokuwa mkubwa hapa Tunduma tunawakatisha tamaa wadau,"alisema Wabara.





Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid (wa tatu kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia) wakiwa wameongana na wageni wengine kupata futari wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake Zanzibar. Hafla hiyo ilifanyika Hotel Verde na ilihudhuriwa na wageni mbalimbali, wakiwamo mawaziri, viongozi wa dini, wateja, mawakala na wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ‘Hakuna uhaba wa petroli, dizeli Zanzibar’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imesema hakuna uhaba wa nishati ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa visiwani humo licha ya kukabiliwa na bohari ndogo ya uhifadhi wa nishati hiyo.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa mamlaka hiyo, Mbarak Hassan Haji, wakati akitangaza bei za mafuta kwa waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema kuwa tokea Oktoba mwaka jana Zanzibar imeanza kuhifadhi katika Bandari ya Tanga isipokuwa mafuta ya taa pekee ambayo yanatumika kwa kiwango cha chini.

Alisema kuwa katika Bandari ya Tanga kuna uhifadhi mkubwa wa mafuta ambayo ina matangi ya kisasa na makubwa.

Alisema tangu bei ya mafuta kuanza kupanda duniani Zanzibar imekuwa na uhakika wa mafuta .

Alisema kuna zaidi ya lita milioni 18,000 ambazo huagiziwa kutoka nje ya nchi kila mwezi kutokana na mahitaji ya mafuta. Akizungumza kuhusu bei mpya ya mafuta iliyoanza juzi, alisema bei ya nishati hiyo imeendelea kuongezeka kwa mwezi huu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo gharama za usafirishaji.

Aidha, alisema bei ya petroli kwa mwezi huu wa Aprili ni Sh. 2,642 kutoka Sh. 2,459 ya mwezi uliopita na ni tofauti ya Sh. 183 sawa na asilimia 7.44.

Alisema mafuta ya dizeli yanauzwa Sh. 2,644 kwa mwezi huu kutoka Sh. 2,500 ya mwezi uliopita tofauti ya Sh. 144 sawa na asilimia 5.8.

Alisema mafuta ya taa bei ya rejareja ni Sh. 2,173 kutoka Sh. 1,811 ya mwezi uliopita tofauti ya Sh. 362 sawa na asilimia 20.

Mbarak alisema kuwa sababu zilizopelekea kupanda kwa bei hizo ni pamoja na kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika soko la dunia pamoja na soko la ndani kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Alisema ZURA inapanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi uliopita ili kupata kianzio cha kufanyika mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu.

Alisema pia huangalia gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam, kuangalia thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa Dola za kimarekani, gharama za usafiri, bima na premium hadi Zanzibar, kodi za serikali na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Hata hivyo, alibainisha kuwa pamoja na bei hizo kuongezeka katika soko la dunia kwa mwezi huu serikali inaendelea kupunguza makali ya bei kwa kufidia jumla ya Sh 250 kwa kila lita ya mafuta.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali ili kuepuka kuuziwa magendo na kudai risiti ambayo itawasaidia wanapopata matatizo kupata haki yao.

# NBC yaandalia wateja wake futari

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeandaa hafla ya futari kwa ajili ya wateja wake visiwani Zanzibar, huku Spika wa Baraza la Wawakilishi Zubeir Ali Maulid akiipongeza benki hiyo kutokana na ushirikiano inaoutoa katika nyanja mbalimbali ikiwamo kijamii na kiuchumi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo iliyofanyika Hotel Verde, Zanzibar, Spika Zubeir alionyesha kuridhishwa na namna benki hiyo inavyoshirikiana na Baraza hilo pamoja na serikali katika kuleta maendeleo visiwani Zanzibar kupitia mipango yake mbalimbali ikiwamo ile inayogusa moja kwa moja ustawi wa jamii pamoja na serikali.

“Pamoja na yote hayo niwapongeze NBC kwa kuonesha umuhimu wa wateja wake kwa kurejesha miongoni mwa faida wanazozipata kwa namna mbalimbali ikiwamo kwa njia hii ya kufutarisha na kutoa huduma nyingine mbalimbali kwa jamii...tunashukuru,” alisema.

Awali, akizungumza katika hafla hiyo ya futari, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi alisema benki hiyo imeamua kuandaa futari hiyo ili kujumuika na wateja wake kama hatua ya kuonyesha mshikamano na umoja katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema benki hiyo inaheshimu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutokana na kwamba ni kipindi ambacho mwanadamu anajiweka karibu na Muumba wake kupitia mfungo na kufanya maombi.

“Huu ni mwezi ambao pia unatukumbusha kufanya kilicho chema mbele za Mungu wetu. Kwa kuwa NBC siku zote tupo karibu na imani za wateja wetu tumeamua kuandaa futari hii ili kujumuika na wenzetu kufanikisha hilo,” alisema Sabi.

Alibainisha kuwa benki hiyo ina huduma maalum inayojikita katika kutoa huduma kwa wateja wake wa imani ya Kiislamu, ijulikanayo kama Islamic Banking inayopatikana kwenye matawi yote ya benki hiyo ikiendeshwa katika misingi ya dini hiyo na huduma mbalimbali za mikopo ya riba.

Sabi aliwaomba wale ambao hawajajiunga na benki hiyo kufungua akaunti zao ili waweze kufurahia huduma bora na za kipekee zinazotolewa katika matawi yote ya NBC nchini.

Hafla hiyo ya futari ilihudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwamo mawaziri, viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa, wateja, mawakala pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo.

# Makamu wa Pili ataka makandarasi walipwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla ameutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha makandarasi wanaodai fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule wanalipwa haraka ili kuwapa fursa ya kuendelea na miradi hiyo.

Hemed alieleza hayo katika muendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Magharibi B Unguja inayojengwa kwa fedha za kupunguza athari za UVIKO-19.

Alisema fedha za miradi hiyo zipo kwa ukamilifu, hakuna sababu ya kuchelewesha malipo kwa wakandarasi waliokwisha omba fedha hizo kisheria.

Alisisitiza kuwa serikali haitamvumilia mtendaji yeyote atakaechelewesha utoaji wa fedha za miradi hiyo na kumchukulia hatua za kisheria atakaehusika na tabia hiyo.

Katika ziara hiyo Makamu wa Pili alitembelea eneo linalojengwa maduka kwa ajili ya vifaa vya umeme vilivyotumika lililopo mtaa wa kwa Mchina ambalo hatua ya awali litajengwa kwa fedha za ahueni ya UVIKO-19 na kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi B kutafuta njia ya kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo la ghorofa nne.

Pia, alitembelea ujenzi wa hospitali ya wilaya iliyopo Mwanakwerekwe na kuwahakikishia wananchi wa Zanzibar kuwa hospitali hiyo itakapokamilika itakuwa na wataalamu wa kila fani ili kurahisisha huduma kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema, kukamilika kwa hospitali hiyo kutazalisha ajira mbalimbali za madaktari watakaohudumia hospitali hizo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magharibi B, Hamida Mussa Khamis, alisema Ofisi ya Wilaya ya Magharibi B imejipanga kuhakikisha miradi inakamilika kwa ubora na kwa wakati.

Alisema wananchi wa wilaya hiyo wanauhitaji mkubwa wa sekta ya elimu na ya afya na kueleza kuwa hospitali hiyo itamaliza changamoto ya kukosa huduma mbalimbali hasa za kina mama.

Kwa upande wake Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU), Kanali Makame Abdalla Daima, alisema kuwa ujenzi wa madarasa ndani ya Wilaya ya Magharibi B utakamilika ndani ya wiki tatu zijazo na kuomba uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, waendelee kutoa ushirikiano kwa kufikia hatua hiyo.

# Maelfu ya wanakijiji Hanang wapata majisafi

Na Mwandishi Wetu

ZAIDI ya wanakijiji 4,000 wa Bassotu wilayani ya Hanang Mkoa wa Manyara, wamenufaika na mradi mpya wa majisafi na salama uliofadhiliwa na Serengeti Breweries Limited (SBL), Shirika la WaterAid na Serikali ya Tanzania baada ya kukabidhi kisima cha maji.

Kisima hicho kilichoongezewa ufanisi kitakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi 14,000, katika vijiji vinne vya Bassotu, Dangaida, Viendamudiga na Dilna katika Kata ya Bassotu.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Janeth Mayanja, aliipongeza SBL kwa kuwa mstari wa mbele katika kutoa msaada kwa wakati kwenye miradi ya maendeleo ya jamii katika maeneo na sekta nyeti nchini.

Alisema: "Mradi huu ni mwokozi wa maisha kwa watu wa Bassotu, na nina imani wanakijiji watauhifadhi na kuulinda kwa ajili ya vizazi vyao vijavyo. Ninataka kuwashukuru SBL kwa kujitolea kwao."

Mkurugenzi wa Mahusiano wa Kampuni ya SBL, John Wanyancha, alisema: "Mradi huu wa maendeleo wa 'Maji ya Uhai' umefanywa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na WaterAid Tanzania ili kuboresha afya, kuongeza tija kiuchumi, kuwezesha wanawake na kuwasaidia watoto wa kike kupata muda zaidi shuleni kwa sababu sasa, hawahitaji tena kusafiri kwa saa nyingi kutafuta maji safi."

Mkurugenzi Mkaazi wa WaterAid Tanzania, Anna Mzinga, alisema: "Tutaendelea kuja na mawazo mapya ili kupata masuluhisho ya kibunifu katika ngazi ya kitaifa na kimataifa ili kuwapatia watu maji safi na salama.

Tutahakikisha kila mtu kila mahali anapata kile ambacho wengi wetu tuliokuwa mijini tunapata ambacho ni maji safi na salama." alisema Mzinga.

Aliongeza kuwa usambazaji wa maji kutoka Ziwa Bassotu kwenda kwa jamii ulihitaji matibabu ya haraka baada ya vipimo vya maabara kubaini kuwa kiwango cha madini ya floride kwenye maji kilikuwa juu ya viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Mradi huo ulioweka uwezo wa kutibu maji wa lita 900,000 kwa saa 12 unatosha kukidhi na kuzidi wastani wa mahitaji ya maji ya kila siku ya kata ya Bassotu ambayo ni lita 700,000.

# Waziri awa mbogo kwa wanaovamia hifadhi

Na Munir Shemweta, MUSOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk Angeline Mabula, ametoa onyo kwa wananchi wanaotumia hisani ya Rais, Samia Suluhu Hassan, kuvamia maeneo ya hifadhi yaliyomegwa na kurejeshwa kwa wananchi kutokana na kuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi.

"Na nitoe tahadhari kumekuwa na tabia leo serikali inakumegea halafu kesho unategemea tena utamegewa, hapatakuwa na kubadilisha mipaka au kumega tena maeneo yaliyotolewa, kilichofanyika ni hisani ya Mh. Rais Samia kuridhia lifanyike jambo hilo, lakini siyo ada kila watu wakihitaji wanamegewa," alisema Dk. Mabula.

Alisema timu ya mawaziri wa wizara za kisekta ikiongozwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi iko katika awamu ya pili ya ziara kwenye mikoa mbalimbali nchini kupeleka mrejesho wa uamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975.

Alisema kinachohitajika kwa maeneo yote yaliyomegwa kwa ajili ya shughuli za wananchi ni kuandaliwa mpango wa matumizi mazuri na jukumu la mikoa ni kuhakikisha mipango ya matumizi bora ya ardhi inaandaliwa kwa maeneo yote yaliyomegwa.

Akizungumza na uongozi wa Mkoa wa Mara April 9, 2022 wilayani Musoma, Dk Mabula ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri wa Wizara za Kisekta alisema, mkoa huo pekee ulikuwa na vijiji 19 na mtaa mmoja wenye migogoro ya matumizi ya ardhi na kubainisha kuwa vijiji 19 katika mkoa huo vitaendelea kubaki na kufanyiwa marejeo huku mtaa mmoja ukifanyiwa tathmini.

Kwa mujibu wa waziri huyo , kazi inayofanyika katika kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ni pamoja na kubadilisha maeneo ya hifadhi yaliyopoteza sifa, kurekebisha mipaka kati ya hifadhi za misitu, wananchi na wanyama ambako kuna mwingiliano ili kuweka alama zitakazoonekana ambazo kila mmoja ataheshimu.

Kwa upande wao, Mawaziri wa Wizara za kisekta walisisitiza umuhimu wa uongozi wa mkoa kuanzia ngazi za chini hadi juu kuhakikisha unasimamia vyema sheria ili maeneo ya hifadhi yasivamiwe tena sambamba na kutilia mkazo uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji na kuwapo mipango ya matumizi bora ya ardhi.

" Elimu ya utunzaji vyanzo vya maji itolewe kwa wananchi kwa kuwa wananchi wamekuwa wakifanya shughuli kwenye vyanzo vya maji na hivyo kuathiri vyanzo hivyo na wakati mwingine kuvikausha hasa nyakati za kiangazi" alisema Mhandisi Marypricsa Mahundi.

Kwa upande wake Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Khamis Chillo, alitaka wananchi kupewa taaluma ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

"Wananchi waelimishwa namna bora na sahihi ya matumizi ya ardhi kwa kuwa kuna shughuli nyingi za kibinadamu zinazofanywa katika ardhi na inawezekana zinafanyika kutokana na watu kutofahamu matumizi sahihi ya ardhi, lengo letu ni kupunguza migogoro ya ardhi," alisema Chillo.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi utasababisha baadhi ya maeneo kutengwa na kuwekewa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kusaidia kupunguza changamoto za ardhi.

Mary Masanja aliwaambia viongozi wa mkoa na wilaya wa Mkoa wa Mara kuwa, maeneo yanayomegwa kwa ajili ya wananchi yalikuwa sehemu ya maeneo yaliyohifadhiwa hivyo , wananchi wajiandae kukutana na changamoto za wanyama na kuwataka viongozi kutoa elimu kwa wananchi ya namna ya kuishi maeneo hayo.



Mtaalam wa mifumo ya kompyuta kutoka kampuni ya Vodacom Tanzania PLC, Erick John akitoa maelezo kwa wanafunzi wa shule ya sekondari Omumwani wilayani Bukoba namna ya kutumia tovuti ya E- Fahamu inayowezesha wanafunzi kupata elimu na maudhui kidijitali mahali popote walipo, mafunzo hayo yaliandaliwa na Asasi ya Vodacom Tanzania Foundation ambayo hivi karibuni imetoa msaada wa kompyuta na pia itaunganisha shule 50 za umma zilizoko katika mikoa 10 nchini (School Connectivity Project ). Mafunzo hayo yalifanyika mkoani Kagera hivi karibuni.

# Mil. 475/- zilivyorahisisha huduma afya Moro

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

WANANCHI wanaoishi kwenye kata sita za Manispaa ya Morogoro wameanza kupata huduma bora za afya karibu na makazi yao, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa zanahati hizo uliogharimu Sh. milioni 475. 4.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Michael Waluse, alisema ukaguzi wa miradi ya zahanati hizo zilizojengwa eneo la Mgaza iliyopo kata ya Mindu na kata zingine ni Sultan Area, Mbuyuni, Tungi, Kihonda Maghorofani na Kiwanja cha Ndege.

Waluse alisema jumla ya Sh. 475,432,391.50 zimetumika kwenye ujenzi wa zahanati hizo na kati ya hizo Sh. 379,554,891.50 sawa na asilimia 75 zimetokana na mapato ya ndani na asilimia 21 kutoka serikali kuu.

Alisema tayari manispaa imewapanga watumishi 18 katika zahanati zote sita wakiwamo wauguzi 12 ,madaktari wasaidizi wawili na tabibu wawili ikiwa ni asilimia 20 ya mahitaji ya watumishi 15 kwa kila zahanati.

" Tayari zahanati mpya sita za Manispaa ya Morogoro zimeanza kutoa huduma na ndani ya siku 7 hadi 10 tutahakikisha huduma zote muhimu zinazotakiwa kutolewa zinapatikana" alisema Waluse .

Akizungumzia vifaa tiba alisema baadhi vimepatikana kwa kushirikiana na Ofisi ya Mganga Mkuu wa Manispaa na kutoka vituo vya kutolea huduma za afya 13 vilivyochangia upatikanaji wa meza 32 zenye gharama ya Sh milioni 2. 6.

Alisema hadi sasa jumla ya vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 11. 051 vimepelekwa katika kituo kimoja ikiwa ni asilimia 13 ya mahitaji yote yanayohitajika katika vituo vyote sita na hivyo kuwa na upungufu asilimia 87.

Waluse alisema juhudi zinafanyika ili kukabiliana na upungufu huo ambapo vifaa tiba aina mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 36.9 vimeagizwa kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) .

Kwa upande wa Mganga Mkuu wa Manispaa ya Morogoro, Charles Mkombachepa alisema juhudi mbalimbali zinafanyika ili kuhakikisha vituo hivyo, vinapata dawa kwa kuwa bado havina akaunti ya MSD.

Dk Mkumbachepa alisema baadhi ya vituo vya kutolea huduma vimechangia upatikanaji wa dawa zenye thamani ya Sh. milioni 3. 2 sawa na asilimia tatu ya mahitaji katika vituo hivyo sita na hivyo kuwa na upungufu wa asilimia 97.

## HABARI KIMATAIFA

### MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Zelensky: Hatutaki kupoteza fursa likiwepo suluhisho la kidiplomasia

**Kyiv, UKRAINE**

"HAKUNA anayetaka kujadiliana na mtu au watu waliolitesa taifa hili. Yote yanaeleweka. Na kama mwanaume, kama baba, ninaelewa hili vizuri. Lakini hatutaki kupoteza fursa, ikiwa zipo, kwa suluhisho la kidiplomasia."

Ni kauli ya Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky mwishoni mwa wiki, akisema msimamo wake bado ni kuhimiza amani ingawa Russia, inashambulia raia wake, jambo linaloshangaza dunia, akiomba kupatiwa silaha zaidi kukabiliana na mashambulizi Mashariki mwa nchi yake.

Zelensky ameyasema hayo kwenye mahojiano na shirika la habari la Associated Press (AP), akiwa mjini Kyiv, siku moja baada ya taarifa ya kwamba, takriban watu 52 wameuawa katika mgomo wa kituo cha treni katika mji wa Mashariki mwa Kramatorsk.

Akiwa katika ofisi yake Ikulu, huku madirisha yamewekewa mifuko ya mchanga na kuzingirwa na wanajeshi waliobeba silaha nzito, anasema:

"Tunapigana, lakini kwa ajili ya uhai, huwezi kupigana tu bila kuwapo watu. Ndiyo maana ni kwa nini kuna umuhimu wa kusimamisha hii vita," Zelensky amesema.

Wakati akisema hayo, vikosi vya Russia, vinajikita eneo la mashariki mwa Ukraine, Donbas na Mariupol.


"Tunapigwa. Tunapigana. Tuko imara. Na tukiacha tu tutakuwa kwenye upande dhaifu," amesema.

Zelensky anasema anaamini Waukraine watakubali suala la amani ingawa wamepita mashambulizi ya takribani wiki sita sasa.

Pamoja na matarajio ya amani, Rais Zelensky anasema ameendelea kupokea ushirikiano kutoka nchi za Ulaya ikiwamo Marekani.

Jirani yake, nchi ya Slovakia, ilimpatia mtambo wa kulinda mashambulizi ya anga 'Soviet-era S-300 air defense'.

Aidha, Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson alifanya ziara ya kushtukiza mjini Kyiv, na kuonana na Rais Zelensky, na kufanya mazungumzo.



Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, akizungumza katika mahojiano na shirika la habari la Associated Press (AP), ofisini kwake mjini Kyiv, nchini humo, mwishoni mwa wiki. Rais Zelensky anasema msimamo wake ni amani licha ya mashambulizi ya Russia dhidi ya raia wa nchi yake. **PICHA:MTANDAO**

### UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:

# Ruto aibuka na kibao 'Sipangiwi', tume yaonya neno lililotumika

**Nairobi, KENYA**

SAA chache baada ya Tume ya Kitaifa ya Uwiano na Utangamano wa Kitaifa (NCIC) kuorodhesha neno 'hatupangiwi' kuwa miongoni mwa maneno na misemo ambayo huenda ikaeneza chuki wakati Kenya, ikijiandaa na uchaguzi mkuu, Naibu Rais (DP) William Ruto ametoa remix ya wimbo maarufu uitwao 'Sipangiwi'.

Mwezi uliopita, wakati DP ilipotambulishwa kama mgombea urais wa chama cha United Democratic Alliance (UDA), alicheza na wimbo ambao sasa unaimbwa na wasanii wa Kenya, Exray 'Taniua' na Trio Mio.

Wimbo huo maarufu hutumika sana kwenye mikutano yake.

Neno 'Sipangiwi (hakuna anayenipangia), lililomo kwenye kamusi, sasa limepata umaarufu katika lugha za kisiasa nchini Kenya.

Labda kwa kutambua hilo, na jukumu lake katika matamshi ya sasa ya kisiasa, Mwenyekiti wa NCIC, Mchungaji Samuel Kobia mwishoni mwa wiki, alijumuisha neno hilo kati ya maneno ambayo yanachukuliwa kuwa matamshi ya kisiasa ya chuki.

Maneno mengine kwenye orodha yaliyotolewa na tume hiyo ni pamoja na 'madoadoa', neno ambalo hivi majuzi lilimweka kinara wa ODM Raila Odinga matatani, jambo ambalo huenda likazua mifarakano miongoni mwa jamii na wafuasi wa kisiasa wa vyama mbalimbali.

"Tunajua kwamba mauti na uzima huwa katika ulimi. Tume imeainisha maneno ambayo yamekuwa yakitumika mara kwa mara katika nyanja ya kisiasa ya Kenya kwa nia ya kuibua vurugu miongoni mwa jamii zenye mitazamo tofauti ya kisiasa," amesema Mwenyekiti huyo.

Mwaka jana, DP, katika hafla ya kudhihirisha madai yake kuwa yeye ni mtu wa kujitengenezea mambo yake, alitumia maneno sipangiwi.

"Vile Wakenya wamesema hawapangiwi na mimi nataka niwaambie, mimi kama 'hustler' sipangiwi. Wao wanaweza kupangwa na 'deep state', wapangwe na 'system', lakini sisi hatupangiwi," alidai Ruto.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

HABARI MICHEZO

# FIFA YARUHUSU RASMI MTIBWA KUMTUMIA KANDA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), limeiruhusu klabu ya Mtibwa Sugar kumtumia mchezaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Deo Kanda ambaye hajaichezea timu hiyo tangu aliposajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Msemaji wa klabu hiyo Thobias Kifaru, amesema tayari wamepata Uhamisho wa Kimataifa (ITC), kutoka Fifa, baada ya klabu yake ya TP Mazembe kushindwa kutekeleza jambo hilo kwa wakati.

"Lile suala lililokuwa likiuliziwa sana la Deo Kanda, limemalizika kwani Fifa imetuwashia taa ya kijani kumtumia kwa sababu timu yake iliyokuwa ikimmiliki TP Mazembe iliweka ngumu, na ikawa tabu sana kupata ITC. Tulivyoona hivyo tukapiga hodi huko, nashukuru sasa wameturuhusu.

"Nadhani kilichobaki sasa ni taratibu tu za ki inchi, kwa sababu hawezi kucheza bila kupata vibali vya kufanyia kazi nchini, na kila kitu kikienda sawa, basi anaweza kuonekana kwenye mechi ya Jumapili kati yetu na Dodoma Jiji," alisema Kifaru.

Kanda, anacheza nafasi ya winga wa kulia, akiwa pia ameshawahi kuichezea Simba kwa mkopo akitokea TP Mazembe mwaka 2019, kwa msimu mmoja, kabla ya kurejea tena kwenye klabu yake mama.

Alisajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili, lakini kukazuka sakata, kwani klabu ya Kitayosce FC ambayo ipo kwenye Ligi ya Championship, nayo ikadai imemalizana naye, kitu kilichosababisha mgogoro na kushindwa kuonekana dimbani.

Hata hivyo, Kanda anaikuta Mtibwa ikiwa kwenye nafasi ya 14, na pointi 20 kwa mechi 19 ilizocheza hadi sasa.

MSHINDI...




Mshindi wa kwanza wa kilometa 21, Shmeeza Mukhi, akimaliza mbio zake za kuchangia na kuwapa matumaini watoto wenye mahitaji maalum nchini. Mbio hizo zilifanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Prisons kutafuta 'pumzi' Zambia

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Patrick Odhiambo, amesema kesho, Jumanne wanatarajia kucheza mechi ya kirafiki na moja ya timu kutoka Zambia kwa ajili ya kujiandaa na michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyopo mbele yao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Odhiambo alisema wamepeleka maombi katika timu mbili zinazoshiriki Ligi Kuu Zambia kwa ajili ya kupata mechi ya kirafiki ili kujipima nguvu kabla ya kucheza dhidi ya Coastal Union.

Alisema anatarajia mechi hiyo ya kirafiki kumpa mwanga wa kuona mapungufu ya kufanyia kazi katika kikosi chake kipindi cha mapumziko kabla ya ligi hiyo kuendelea.

"Katika msimamo tuko katika nafasi mbaya sana, jambo kubwa kwa sasa ni kuhakikisha tunapata mechi ya kirafiki kuona wapi tunatakiwa kufanyia kazi kuhakikisha tunarejea katika ligi tukiwa fiti na kutafuta matokeo ya ushindi katika michezo iliyopo mbele yetu ya mzunguko wa pili," alisema.

"Kazi ninayoifanya ni kuwajenga kisaikolojia wachezaji wangu na kupunguza presha waliyokuwa nayo kwa sababu tunashika nafasi ya chini katika msimamo wa ligi hiyo," alisema Odhiambo.

Alisema malengo makubwa kwa sasa ni kuhakikisha wanashinda mchezo wao ujao dhidi ya Coastal Union watakaocheza nyumbani ili kupata pointi tatu muhimu zitakazowasaidia kutoka chini.

"Najitahidi kupunguza presha kwa wachezaji wangu kwanza tukipata hii mechi ya kirafiki itatusaidia lakini lazima tuhakikishe tunashinda mechi yetu dhidi ya Coastal Union kutoka katika nafasi ya chini ya msimamo,"alisema kocha huyo.

Tanzania Prisons ambayo itashuka dimbani Aprili 18, mwaka huu dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, inashika nafasi ya 15 ikiwa ya pili kutoka mkiani baada ya kujikusanyia pointi 16 pekee katika mechi 19 ilizocheza hadi sasa.

# Betika kulipia mashabiki 24 mechi Simba, Yanga

**Na Saada Akida**

MASHABIKI 24 wa timu za Simba na Yanga wamepewa fursa ya kushuhudia mechi ya Ligi Kuu Bara ya watani hao wa jadi bure, itakayopigwa Aprili 30, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, imeelezwa.

Mashabiki hao ni wale watakaoibuka washindi kwenye droo ya Mtoko wa Kibingwa inayoendelea nchini ikiendeshwa na Kampuni ya Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Betika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Masoko wa Kampeni ya Betika, Nelson Mwanuzi, alisema wametoa fursa kwa mashabiki wa timu hizo kushuhudia mchezo huo wa watani wa jadi bure, huku gharama zote zikiwa juu ya kampuni hiyo.

Alisema hadi sasa wamepatikana washindi 10 kutoka mikoa ya Dodoma, Mtwara, Morogoro, Mbeya, Mara na Tabora, huku zikiwa zimesalia nafasi 14 kwa mashabiki kushuhudia mechi hiyo ya watani kwa kucheza katika droo ya Mtoko wa Kibingwa.

Aliwataja washindi hao kuwa ni Emmanuel Zadie na Amos Mdao (Dodoma), Hamidu Hassan na Sharafi Sharkati (Mtwara), Michael Richard, Patrick Ngwala na Ibrahim Kondo (Morogoro), Dominick Mwakalinga (Mbeya), Lameck Mbusiro( Mara) na Hamis Omary wa Tabora.

"Wote watagharamiwa tiketi za ndege kwenda (Dar es Salaam na kurudi mikoa wanayotoka0 kushuhudia mechi hiyo, watalala hoteli ya nyota tano wakiwa Dar es Salaam na watalipiwa tiketi za jukwaa kuu uwanjani kwa ajili ya kushuhudia mchezo huo," alisema Mwanuzi.

Alisema ili kupata fursa hiyo, washiriki wanatakiwa kucheza kwenye droo ya Mtoko wa Kibingwa kujishindia tiketi hiyo adhimu, nafasi 14 bado ziko wazi na rahisi kwa kuanzia Sh. 1,000 na kwamba ukichezwa kwenye droo ya Mtoko wa Kibingwa ni rahisi kushinda.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE KUBAKI PSG
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, anatarajia kubaki Paris Saint-Germain, huku Real Madrid sasa wakijiandaa kumshawishi straika wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. ***(Sunday Mirror)***

### TCHOUAMENI AITAKA MADRID
ERLING Haaland na kiungo wa Monaco mwenye umri wa miaka 22, Aurelien Tchouameni wanataka kusajiliwa Real Madrid. ***(AS)***

### CONTE KUSAJILI MSHAMBULIAJI
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte anataka kumsajili mshambuliaji namba 10 kipindi cha majira ya joto ili kumruhusu Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, kucheza kama straika. ***(Mail on Sunday)***

### ARSENAL, SPURS KWA MADDISON
KLABU za Tottenham Hotspur na Arsenal zipo kwenye mbio moja kuwania kumsajili kiungo wa Leicester na England, James Maddison mwenye umri wa miaka 25. ***(Sun on Sunday)***

### GERRARD AJIPANGA KUSAJILI
KOCHA wa Aston Villa, Steven Gerrard, anapanga kufanya usajili mkubwa wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto huku akiuza nyota nane. Mlinzi wa Liverpool, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 24, Yves Bissouma wa Brighton mwenye miaka 25, ni miongoni mwa wanaowaniwa na Gerrard. ***(Sunday Mirror)***

### INTER YAMTAKA LUKAKU
KLABU ya Inter Milan inawania kumsajili straika wa UBelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, kutoka Chelsea kipindi cha majira ya joto - lakini kwa mkopo. (Football Insider)

### JORGINHO ATAKIWA JUVE
KLABU ya Juventus inawania kumsajili kiungo wa Chelsea na Italia mwenye umri wa miaka 30, Jorginho. ***(Tutto Mercato)***

### BREMER AWANIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL ipo kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa kati wa Torino, mwenye umri wa miaka 25, Gleison Bremer, lakini wanakabiliwa na upinzani kutoka Inter Milan. ***(Goal)***

### TIELEMANS ANUKIA UNITED
MATUMAINI ya Manchester United kumsajili kiungo wa Leicester City, Youri Tielemans yameongezeka baada ya Liverpool na West Ham kujitoa kwenye mbio za kumuwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(CBS Sports)***

### VAN PERSIE KUMSAIDIA HAG
ERIK ten Hag anataka kumfanya mchezaji wa zamani wa Manchester United, Robin van Persie kuwa msaidizi wake wakati atakapochukua mikoba ya kuinoa klabu hiyo ya Old Trafford. ***(Mail on Sunday)***

### RANGERS KUMUACHIA DIALLO
KLABU ya Rangers haina mpango wa kuongeza muda wa mkopo kwa mchezaji, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 19 kutoka Manchester United baada ya msimu huu. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AMUOMBA RADHI SHABIKI UNITED IKICHAPWA

Siku zote tunapaswa kuwa na heshima, subira na kuweka mfano kwa vijana wote, hivyo ningependa kuomba...

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Cristiano Ronaldo ameomba msamaha baada ya kuonekana kugonga simu kutoka mkononi mwa shabiki baada ya kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

Picha ziliibuka kwenye mitandao ya kijamii zikimuonyesha Ronaldo akitelezesha mkono wake kuelekea chini alipokuwa akitoka nje ya uwanja pale Goodison Park.

Walioshuhudia walisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, aligonga simu ya shabiki kutoka mkononi na ikaanguka chini.

"Si rahisi kushughulika na mihemko katika nyakati ngumu kama zile tunazokabiliana nazo," alisema Ronaldo.

"Hata hivyo, siku zote tunapaswa kuwa na heshima, subira na kuweka mfano kwa vijana wote wanaopenda mchezo huu mzuri.

"Ningependa kuomba radhi kwa hasira yangu na, ikiwezekana, ningependa kumualika shabiki huyu kutazama mchezo kule Old Trafford kama ishara ya mchezo wa haki na uanamichezo."

Ronaldo, mfungaji bora wa United msimu huu, alirejea katika timu ya United baada ya kukosa sare ya bao 1-1 na Leicester City wikendi iliyopita kutokana na kuugua.

Hata hivyo, hakuweza kuiwezesha timu hiyo kupata ushindi dhidi ya Everton waliokuwa kwenye hatari ya kushuka daraja.

Kipigo hicho kimeifanya United kuwa nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na wanakabiliwa na uwezekano wa kushindwa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kwa kuwa wapo nyuma ya Tottenham Hotspur kwa pointi sita.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

BOLOGNA

VERSUS

SAMPDORIA

1 | 2.17

X | 3.25

2 | 3.30

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka


SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARSENAL HATIHATI KUFUZU UEFA



**LONDON, England**

ARSENAL iliteleza kwa kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Brighton katika Uwanja wa Emirates Jumamosi huku matumaini yao ya kumaliza katika nafasi nne za juu yakipata pigo kubwa.

Leandro Trossard na Enock Mwepu walifunga bao katika kila kipindi na ingawa Martin Odegaard alirudisha bao moja baadaye, vijana wa Mikel Arteta walipata kipigo chao cha pili mfululizo kwenye Ligi Kuu England.

Brighton walikuwa wameshindwa kufunga katika mechi zao tatu zilizopita, lakini walionyesha mchezo mzuri na kupata ushindi wao wa kwanza wa ligi ugenini tangu Februari.

Arsenal wamebaki katika nafasi ya tano, lakini wamepitwa pointi tatu na wapinzani wao Tottenham Hotspur ambapo vijana hao wa Antonio Conte walipata ushindi dhidi ya Aston Villa.

"Imekuwa wiki ngumu; haswa leo kwa sababu tulitaka majibu (ya kushindwa kule Crystal Palace)," alisema Arteta akiiambia BBC baada ya mchezo huo.

"Ilikuja kipindi cha pili, ambacho kimechelewa sana; tunapaswa kuwa na ujasiri na utulivu ili kucheza vizuri zaidi na kuongeza kiwango katika kipindi cha kwanza.

"Tulikuwa wazembe, hatukuwa na lengo la kushambulia, tulikuwa wajinga na hatukutaka kucheza mbele.

"Tumeonyesha kwa wiki nyingi jinsi tunaweza kucheza vizuri; imekuwa wiki ngumu na tumepoteza wachezaji wakubwa, lakini ukipata kile unachotaka, si kila kitu kitakuwa na anga ya bluu. Hii ni timu yetu katika wakati mzuri na haswa kushindwa.

"Kuna michezo mingi ya kucheza lakini inabidi tuwe na wasiwasi kuhusu uchezaji huo, hasa kipindi cha kwanza."

# Ancelotti: Nitaendelea kumchezesha Bale

**MADRID, Hispania**

CARLO Ancelotti alisifu ustadi wa Gareth Bale baada ya mchezaji huyo wa Wales kuzomewa na baadhi ya mashabiki wa Real Madrid wakati wa ushindi wa Jumamosi dhidi ya Getafe.

Bale aliingia akitokea benchi dakika ya 74 wakati wa ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, akimalizia pasi nne kati ya tano na kupiga mashuti mawili, moja lililomjaribu kipa wa Getafe, David Soria.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amewagawa mashabiki katika mji mkuu wa Hispania, akifunga mabao muhimu na kushinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika muda wake hapo, lakini amekosa muda mwingi wa kucheza kutokana na majeraha katika miaka ya hivi karibuni.

Bale pia amefahamisha kuwa anapendelea kuichezea Wales kuliko klabu yake, na anatarajia kumaliza miaka yake tisa hapo Madrid wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa mchezo huo, Ancelotti alikataa kuwakosoa mashabiki, lakini alimsifu Bale na kusisitiza kuwa ataendelea kucheza iwapo anafaa.

"Mashabiki ni muhimu sana, kama vile dhidi ya PSG," alisema, akirejelea mabadiliko wakati wakipata ushindi wa jumla wa mabao 3-2 katika hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain.

"Bale alizomewa, lakini ni mchezaji muhimu na makini na kama yuko vizuri ataendelea kucheza."

Mabao ya Casemiro na Lucas Vazquez yalihitimisha ushindi huo, ambao ulirejesha uongozi wa Madrid kwa pointi 12 kileleni mwa LaLiga, na Ancelotti aliridhika na uchezaji wa timu yake, lakini akasisitiza mbio za ubingwa bado hazijakamilika.

"Tuko karibu (na jina)," alisema. "Ni mwendo mzuri lakini bado haujaisha, lazima tuendelee kupambana, tuna mechi mbili za ugenini dhidi ya Sevilla na Osasuna."

Mchezo unaofuata wa 'Los Blancos' hao ni Jumanne dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, ambapo Madrid wanaongoza kwa mabao 3-1 waliyoyapata mchezo wa kwanza.

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# SIMBA HAWATANII KWA ORLANDO

**Na Dennis Fussi**

MWENYEKITI wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, amesema licha ya timu yao kukabiliwa na ratiba ngumu, lakini watajitahidi kuanza mapema maandalizi ya mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates.

Miamba hiyo ya Tanzania itakutana na Orlando Pirates ya Afrika Kusini, mchezo wa mkondo wa kwanza ukipigwa Dar es Salaam Aprili 17 kabla ya kurudiana Aprili 24, mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Mwenyekiti huyo ameeleza mikakati yao ya kuhakikisha wanavuka kigingi hicho, ambacho kimekuwa kikiwashinda kwa misimu miwili iliyopita na kwamba kitu cha kwanza ni kuanza maandalizi mapema.

"Unajua ratiba imekuwa ngumu, tuna mechi za ligi, lakini pia Kombe la FA, kitu cha msingi kwetu uongozi, tumepanga kuzungumza na TFF, ili kutupa muda walau wa wiki moja kwa ajili ya kujiandaa na mechi hizi mbili dhidi ya Pirates," alisema Mangungu.

Mangungu amesema uongozi wao una mpango wa kukutana na wachezaji kwa lengo la kuwajenga kisaikolojia na kuwapa maneno mazuri, ambayo yatawaongezea ari ya upambanaji na kuvuka kikwazo hicho.

Simba iliyopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, jana Jumapili ilishuka dimbani kucheza na Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.




# Azam FC sasa msuli Kombe la FA



**Na Saada Akida**

BAADA ya kutokuwa na mwenendo mzuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Azam FC umehamishia nguvu na jitihada zake katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup.

Azam FC wanashuka dimbani keshokutwa, Jumatano kuwakaribisha Polisi Tanzania katika mchezo huo wa robo fainali ya Kombe la ASFC utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, alisema baada ya kupoteza mechi yao dhidi ya Yanga, sasa wanarejea uwanjani kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chao kuhakikisha wanafanya vizuri katika michuano ya Kombe la Shirikisho.

Alisema ana imani malengo yao katika ligi hayawezi kutimia hivyo watahakikisha wanafanya vizuri katika michuano ya ASFC, kutafuta matokeo mazuri na ushindi kwenye mchezo wa robo fainali dhidi ya Polisi Tanzania.

"Hatuko vizuri kwenye mbio za ubingwa kwa sababu ya walikuwapo juu yetu kutupita pointi nyingi, lakini hatujakata tamaa, tumepoteza dhidi ya Yanga na sasa tunaangalia mechi zilizopo mbele yetu dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Shirikisho," alisema kocha huyo.

Alisema ana imani na wachezaji wake kufanya vizuri katika michezo iliyobaki ya Ligi Kuu, lakini pia kuhakikisha wanapambana kucheza nusu fainali ya Kombe la FA ili kuzidi kusonga mbele kwa kucheza fainali na kuwa miongoni mwa timu zitakazokwenda kuiwakilisha nchini katika michuano ya kimataifa msimu ujao.

Azam FC msimu huu hawajafanya vizuri, kutokana na hadi sasa kushika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 28, pointi 23 nyuma ya vinara Yanga, huku Simba iliyopo nafasi ya pili ikiwazidi pointi 12 kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 11/04/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4556 | Kampala City Council vs Dove All Stars | 1.53 | 3.95 | 6.00 |
| 17:00 | 2080 | FK Tukums 2000/Tss vs Rigas Futbola Skola | 8.17 | 4.76 | 1.30 |
| 18:00 | 1104 | Spartaks Jurmala vs SK Super Nova | 1.81 | 3.51 | 3.80 |
| 18:00 | 1157 | Gaz Metan Medias vs CS Mioveni | 23.71 | 8.50 | 1.09 |
| 18:00 | 2980 | Saint George FC vs Dire Dawa Kenema FC | 1.42 | 4.09 | 6.62 |
| 19:00 | 1191 | Stjordals-Blink vs Sandnes Ulf | 2.73 | 3.22 | 2.37 |
| 19:00 | 1893 | Radomiak Radom vs Jagiellonia | 2.12 | 3.15 | 3.20 |
| 19:00 | 2362 | Kongsvinger IL vs Skeid Fotball | 1.93 | 3.54 | 3.34 |
| 19:00 | 3466 | Montego Bay Utd vs Dunbeholden FC | 3.85 | 2.88 | 2.03 |
| 19:00 | 4089 | Raufoss vs Ranheim | 2.12 | 3.56 | 2.87 |
| 19:00 | 4224 | GKS Tychy vs KS Gornik Polkowice | 1.82 | 3.51 | 3.75 |
| 19:00 | 5314 | IK Start vs Mjondalen | 2.23 | 3.31 | 2.87 |
| 19:00 | 5763 | Stabaek vs Sogndal | 1.72 | 3.70 | 4.00 |
| 19:00 | 5959 | Bryne vs Kfum Oslo | 2.08 | 3.30 | 3.16 |
| 19:30 | 2915 | Radnik Surduluca vs Novi Pazar | 1.73 | 3.41 | 4.39 |
| 19:30 | 4176 | FK Napredak vs Metalac | 1.85 | 3.41 | 3.75 |
| 19:30 | 4850 | Vojvodina vs Proleter | 1.63 | 3.49 | 5.04 |
| 20:00 | 1516 | FC Trollhattan vs Gais | 2.50 | 3.65 | 2.50 |
| 20:00 | 2573 | Vasteras SK vs Ostersunds | 2.36 | 3.33 | 2.98 |
| 20:00 | 3012 | Halmstads BK vs Norrby IF | 1.82 | 3.55 | 4.36 |
| 20:00 | 3046 | Vejle BK vs Viborg FF | 3.14 | 3.29 | 2.21 |
| 20:00 | 4199 | IFK Varnamo vs Sirius FK | 2.43 | 3.17 | 2.68 |
| 20:00 | 4808 | Osnabruck vs Verl | 1.58 | 3.97 | 5.16 |
| 20:00 | 5794 | Tsarsko Selo vs Pirin Blagoevgrad | 2.78 | 3.22 | 2.33 |
| 20:10 | 2756 | Malmo vs Elfsborg | 1.54 | 3.98 | 5.05 |
| 20:30 | 1244 | Eyupspor vs Altinordu | 1.56 | 3.84 | 5.06 |
| 20:30 | 3652 | Sectzya Nes Ziona vs Maccabi Bney Reine | 2.66 | 2.81 | 2.96 |
| 20:30 | 4421 | SC Kfar Qasem vs AS Ashdod | 2.49 | 2.90 | 3.10 |
| 20:30 | 5387 | Maccabi Tel Aviv vs Maccabi Haifa | 2.87 | 3.21 | 2.27 |
| 20:30 | 5484 | Antalyaspor vs Hatayspor | 2.11 | 3.37 | 3.27 |
| 21:00 | 4474 | Steaua Bucuresti vs Voluntari | 1.59 | 3.62 | 5.75 |
| 21:00 | 4988 | Vasas SC vs Szeged | 1.65 | 3.49 | 4.85 |
| 21:05 | 5731 | CA Acassuso vs Ituzaingo | 2.11 | 2.67 | 3.98 |
| 21:20 | 2688 | Hajer Club vs AL Akhdood | 2.21 | 2.87 | 3.35 |
| 21:20 | 3070 | Al Khaleej Club vs Ohud Medina | 2.39 | 2.95 | 3.20 |
| 21:20 | 5922 | AL Sahel SC vs AL Draih | 2.16 | 3.00 | 3.65 |
| 21:30 | 3155 | Justo Jose De Urquiza vs Comunicaciones | 3.91 | 3.13 | 1.91 |
| 21:30 | 4231 | Argentino Merlo vs Central Cordoba | 3.00 | 2.95 | 2.50 |
| 21:30 | 4900 | Waterhouse FC vs Cavaliers FC | 1.44 | 3.99 | 6.43 |
| 21:30 | 5086 | Brescia vs Parma | 1.96 | 3.27 | 3.77 |
| 21:45 | 1705 | Bologna vs Sampdoria | 2.17 | 3.25 | 3.30 |
| 21:45 | 2172 | Huddersfield vs Luton Town | 2.28 | 3.17 | 3.07 |
| 21:45 | 2437 | Sedan vs Concarneau | 3.91 | 2.92 | 2.06 |
| 21:45 | 4848 | Paris FC vs Dijon | 2.01 | 3.17 | 3.76 |
| 22:00 | 1595 | Almeria vs Ponferradina | 1.58 | 3.85 | 5.33 |
| 22:00 | 2827 | Rayo Vallecano vs Valencia | 2.17 | 3.22 | 3.47 |
| 22:00 | 5252 | Al Jabalain vs AL Khlood | 1.71 | 3.31 | 4.67 |
| 22:00 | 5362 | Foggia vs Catanzaro | 2.70 | 3.10 | 2.65 |
| 23:00 | 3291 | Universitario Popayan vs Barranquilla FC | 2.30 | 3.11 | 2.91 |
| 23:05 | 1437 | Defensores Belgrano vs Quilmes | 2.86 | 2.77 | 2.57 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Aprili 11, 20
Nipashe



## Ronaldo amuomba radhi shabiki United ikichapwa



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kulia), akiwania kumiliki mpira dhidi ya beki wa Polisi Tanzania, Yahaya Mbegu, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, Kilimanjaro jana na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YASAFISHA NJIA YA UBINGWA YANGA

●●●Ni wakati Polisi Tanzania ikipata sare ya kwanza kwa Mnyama, Pablo asema akili yote kwa Orlando Jumapili...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza tangu ipande daraja na kucheza Ligi Kuu msimu wa 2019/20, timu ya Polisi Tanzania imefanikiwa kupata sare dhidi ya mabingwa watetezi, Simba baada ya jana timu hizo kumaliza dakika 90 bila kufungana katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, Kilimanjaro.

Ilikuwa ni mechi ya sita kwa timu hizo kukutana kwa misimu mitatu, huku Simba ikishinda mara tano, lakini ilishindwa kufanya hivyo jana.

"Haikuwa rahisi kucheza kwenye uwanja kama huu, akili yetu sasa tumeielekeza zaidi kwenye mechi yetu ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Kocha Mkuu, Pablo Franco baada ya mechi hiyo.

Kwa matokeo hayo, Simba imeachwa kwa tofauti ya pointi 10 na vinara wa Ligi Kuu, Yanga baada ya kila timu kushuka dimbani mara 19. Simba imefikisha jumla ya pointi 41, huku Yanga ikiwa ina pointi 51.

Hata hivyo, Simba itabidi ijilaumu yenyewe kwa kukosa mabao mengi rahisi kipindi cha kwanza, lakini ilikuja kubadilikiwa kipindi cha pili kwani kadri dakika zilivyozidi kusonga mbele, walikuwa hatarini zaidi kupoteza mechi kuliko wao kupata bao.

Polisi Tanzania walianza kwa kulishambulia lango la Simba, na kumfanya kipa Benno Kakolanya kufanya kazi ya ziada alipodaka shuti la karibu la Kassim Haruna, huku dakika ya saba akipangua shuti kali la Daruweshi Saliboko.

Dakika tatu baadaye kona ya Rally Bwalya ilizua kizaazaa kwenye lango la Polisi Tanzania, ambapo wachezaji wa Simba walikuwa wakijigongagonga kukwamisha mpira wavuni, kabla haujaokolewa na mabeki wa timu mwenyeji.

Mastraika wawili wa Simba waliochezeshwa kwa pamoja jana, Chriss Mugalu na Meddie Kagere wangeweza kuiandikia timu yao mabao dakika ya 12 na 14, lakini imekuwa ni gonjwa sugu kwao kukosa mabao ya wazi.

Kagere aliingiziwa krosi na Mugalu dakika ya 12, lakini alitaka kufunga kwa mikogo, badala yake mpira huo ukamgonga kipa Metacha Mnata na kushindwa kuingia wavuni. Mugalu naye akibaki na kipa Metacha, alipiga shuti dhaifu ambalo lilitoka nje.

Polisi Tanzania nusura wapate bao dakika ya 32, baada ya Deusdety Cosmas kumuacha kwa mbio Gadiel Michael na kupiga krosi ambayo ilitambaa kwenye lango la Simba ikiwa inatafuta muunganishaji lakini Tariq Kiakala alichelewa kufika kwenye eneo la tukio.

Licha ya kipindi cha pili timu zote kufanya mabadiliko kadhaa, lakini yalionekana kuisaidia zaidi Polisi Tanzania ambapo kama ingekuwa makini ingeweza kupata angalau bao moja kwenye dakika 15 za mwisho.

Mbali na Vitalisy Mayanga kukosa bao la wazi akijikwaakwaa mwenyewe akiwa amebaki na kipa Kakolanya dakika ya 49, dakika moja kabla ya mechi kumalizika, kipa huyo wa Simba aliinusuru kufungwa baada ya kumzuia Haruna aliyetaka kumpiga chenga wakiwa wamebaki wao wawili tu.

Simba sasa inarejea Dar es Salaam kujiandaa na mechi yake ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates itakayopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa saa 1:00 usiku.

## Yanga SC yapewa angalizo ubingwa



**Na Sanula Athanas, DODOMA**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Yanga, Sekilojo Chambua, amezungumza na Nipashe kuhusu maisha yake ya kisoka, huku akitoa angalizo kwa vinara hao wa Ligi Kuu Bara, kuelekea mbio za ubingwa, lakini pia akaanika mbinu kwa Simba kuimaliza Orlando Pirates katika mechi ya hatua ya robo-fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**UK. 14**

## Azam FC: Msuli sasa Kombe la FA



**Na Saada Akida**

BAADA ya kutokuwa na mwenendo mzuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Azam FC umehamishia nguvu na jitihada zake katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup.

**UK. 23**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >